Appendix

The following appendix includes the untranslated Swahili for every Swahili-language reference made in this thesis. For ease of cross-referencing, it is divided by chapter, and organised within these chapter divisions, by, first, footnote number, then page number and, finally, the source details as they appear in the original footnote.

Introduction

Footnote 110, p.39, *Mambo Leo*, Letter Petro Ulesi Mboga, March 1945, p.34.

Nia yangu kuandika maneno mengi bali Kiswahili chanishinda, kwa hiyo ninayo hakika watu watajito – keza katika gazeti kwa kunijibu. Kwa leo yanatosha.

Chapter One

Footnote 243, p.101, *Mambo Leo*, Letter TML. 79801 A. Majatta, April 1945, p.46.

Neno hilo la barua limewavuta askari waone faida kubwa kwa watoto wanawake wasomeshwe. Askari wengi wangeweza kujipatia barua kwa wake wao; lakini kwamba wengi mno hawajui kusoma, wanakosa barua. Kwa yakini wake wanaojua kusoma ni faraja kubwa kwa waume wanapokuwa safarini. Kwa hiyo ni vema sana wazee wavavute binti sana waende masomoni, au sivyo mbele kutakuwa na hekaheka ya kuja kuwachuja wanawake. Mke anapojua kusoma huwa mwepesi wa kuwakumbuka wa mbali, pia kutazama maagizo ya mume anayomtuma. Basi wazee wa Usambaa, ninawaomba mimi mwana wenu, fanyeni nguvu watoto ndugu wapate mahali na nafasi ya masomo, ulimwengu unakwenda mbele. Watu wengi huona ugumu kutembezewa barua zao kwa kutafutwa watu ovyo wazisome.

Chapter Two

Footnote 36, p.114, *Mambo Leo*, Letter H.M. Mtengeti, August 1946, p.85.

Siku moja nilipokwenda hoteli kunywa chai mjini Dar es Salaam, kwa bahati nikamkuta kijana mmoja wa Kichagga ambaye tulikuwa tukisoma pamoja Old Moshi Secondary School mwaka 1942. Nilipomwamkia akajidai hanijui kabisa. Mimi nikamwuliza, Aisee wewe kabila gani? Akanijibu, Mimi kwetu ni Zanzibar.

Mimi nikazidi kumhoji, Wewe siye fulani tuliyekuwa tunasoma wote Old Moshi? Akasema, Hata kidogo, si mimi. Basi mimi nikamwacha, lakini nikijua kuwa ndiye tu bali anaona haya kutaja kabila lake.

Bada ya dakika chache nikamwona ananiiia na kuniambia. Asiee unisamehe sana, maana kwa kweli naona haya kutaja kabila langu hapa mjini. Basi nikaona ajabu sana, nikamwambia si kitu. Nikampeleka nyumbani kwangu kula chakula. Basi jamani, Waswahili wamesema, Chako ni chako hata kama ni kibaya*. Mwenyezi Mungu alivyokuumba uwe kabila fulani hakuwa mpumbavu, basi yafaa kulipenda kabila lako hata kama halina sifa yo yote.*

Footnote 37, p.114, *Mambo Leo*, Letter Simeon Muya, August 1946, pp.85-6.

Jamaa wengi mijini na kila mara ninapowauliza makabila yao, hujibu ni wa Boma fulani la kwao. Au pengine hutaja kabila fulani lenye utukufu mwingi. Kwa Muha hujitapa ya kuwa kwao ni Kigoma, yaani ndilo kabila lao; ukimkazania hujiita Mmanyema. Vile vile Mnguu ukimwuliza kabila lake hukujibu ya kuwa ni mtu wa Zanzibar au mtu wa pwani, basi kama ukimtoa hapo, ndipo anajisema ni Mkilindi safi. Shida hii imewapata watu wengi wapumbavu wafichao makabila yao, nao baada ya kupatwa na ajali zao ugenini mali zao hurithiwa na maboma ya kwao. Watu kama hawa hutiwa "KOTI JEUSI" au "MATAJIRI WA MCHANA". Ni watu wasio na mawazo yo yote juu ya maisha yao, ila kula na kuvaa tu. Kufuta kabila ndio kufuta ushikamano wa kikabila tuliopewa na Muumba wetu.

Footnote 48, p.117, *Mambo Leo*, Letter T/77616 CMS Abedi M. Fonga, November 1945, p.129.

Dada wa kwetu wameenea kila mahali mbali na kwao. Tena dada hawa wanapata msaada kwa wazizi wao, wanapelekewa hata maharage. Basi ni kosa la wazazi wao; laiti mazazi akimwona binti anafanya ubovu huo akimkaripia, binti hawezi kuendelea kufanya mambo hayo. Huko Nairobi walivyo wengi kama ndiko Bukoba.

Nilimwuliza mmoja ninayemjua kuwa ana mume kwetu, Bibi, nama gani mbona hivi? Bwana yuko wapi? Akajibu, Tutakalia bwana tu; saa ngapi nitapata nguo? Siwezi kungoja kanga 4 mpaka mwisho wa mwezi au shuka moja ya hariri. Mimi sasa napata wiki moja magauni manne na fedha za kunitosha.

Footnote 52, p.117, *Mambo Leo*, Letter T/77616 CMS Abedi M. Fonga, November 1945, p.129.

Basi ninaomba mbele ya serikali na wazee wangu na Wakama wetu, mtuhurumie kwa aibu inayotupata sisi katika nchi za ugenini; Kuitwa shemeji na kila mtu, vichwa vyetu huwa chini kwa huzuni.

Footnote 60, p.119, *Mambo Leo*, Letter T/77616 CMS Abedi M. Fonga, November 1945, p.129.

Wenyeji wakishauriana kuwa mwanamke ye yote akionekana forodhani au kivukoni bila barua ya bwana wake na waraka wa ndoa, arudishwe; Serikali yetu ingepata nguvu ya kuwazuia.

Footnote 84, p.123, *Mambo Leo*, Letter Simeon Muya, August 1946, pp.85-6.

Watu wanaokataa makabila yao, wasidhani ni wastaarabu, maana mtu mstaarabu huwa na asili yake, na kabila lake, na boma lake la kwao. Kundi la watu hao baadhi yao ndio maharamia na malaya na wengine wenye maisha mabovu. Makabila mengi hupata ubovu sana kwa ajili ya watu hawa wasiojua mahali pao, au wanaojificha ili wasijulwe.

Footnote 90, p.124, *Mambo Leo*, Letter Maziku s/o Malongo, January 1946, p.2.

Ndugu Wasukuma na Wanyamwezi wanapofika miji mikubwa hawapendi kusema msemo wa kikwao. Akiamkiwa, Ng'wadila, huitikia Jambo au Good Morning, akizidi kuulizwa, Ulinimanyicha? (unanijua) Oo, unajaa machoni!! Haya mtu mmesoma naye miaka mitatu na zaidi au mmekulia pamoja na kucheza michezo majumbani kwa wazee, misipoonana tena miaka mitatu au zaidi mtasahauliana. Hili sisemi kwa wanaume tu, balu hata wanawake. Ustaarabu sio kusema Kiswahili na Kiingereza, huo ni umoja wa kusikiana mkiwa na lugha za kabila mbali mbali. Mwahuzunisha walimu waliotufunza. Walio na tabia hizo hata wa kabila nyingine nawaomba myaache kabisa. Samahani kwa hayo ndugu.

Footnote 97, p.126, *Mambo Leo*, Letter L. Th. Kimwaga Mpenda, February 1947, p.13.

Ni haki kabisa chifu awe anayejua. Wakubwa wa nchi ni machifu na wafuasi wawasaidiao kuinua raia ni walimu. Hao ndio walezi wanaowasha taa mbele ya watoto raia wa kesho. Basi machifu wategemewao na raia wote wanayo lazima wawe na maarifa na elimu zaidi kuliko raia, ili waweze kuushika usukani na kuelekeza palipo sawa. Machifu wakitulea kwa skuli na elimu yao ilivyo, ndivyo tutakavyokuwa, au kutakuwa ubishi kati ya raia na machifu. Raia kasoma, chifu hakusoma, basi lazima mawazo yapitane.

Ninayo hakika kwa siku hizi wapo machifu vijana ambao wameelimishwa mpaka madarasa ya juu kisha hurithi viti vya wazee wao. Pia kati yao wanajitahidi kutumia elimu yao kuigawa kwa raia. Lakini wengine wao hurudi nyuma baada ya kukikalia kiti, basi elimu anaitupilia mbali na kuchukua sheria na madhehebu ya kikale kwa kuwafuata washauri wake wazee ambao ni pahali pake kuwageuza wao wamfuate, yeye anawafuata kurudi gizani. K.m. humwambia akifuata maneno ya Serikali, raia, watakimbia wahame (b) Kuagiza mganga wa mvua katika nchi na hali yeye amekwisha fundishwa asili ya mvua, na mengineyo mengi humweleza naye huamini na kuyatenda.

Machifu wakisha somea kazi yao wasikubali kurudishwa nyuma tena na hao wazee. Machifu watakuwa na msaada mkubwa kwa kuendesha nchi katika ustaarabu wakishirikiana na walimu. Lililo kubwa ni Machifu wawe wenye kuamuru mambo yatupelekayo kwenye mwanga mkubwa siyo kurudisha utambi ndani ya taa.

Samahani kwa Machifu, siyo kama twawadharau, la, hasha; bali twaomba maendeleo ya kisasa yawe imara na thabiti kwa ajili yao.

Footnote 102, p.126, *Mambo Leo*, Letter N/42663 Sigmn H.K. Salim, October 1946, p.110.

Katika nchi Usambaa uchifu hufuata ukoo wa Wakilindi. Jambo hilo huleta fitina katika nchi nzima, kwamba wako watu walio na elimu ya kutosha lakini hawawezi kupewa utawala ila awe ni wa ukoo wa Wakilindi. Kwa yakini ingefaa machifu wawe ni watu waliosoma sana, si kumchagua mtu asiyejua lo lote.

Tazama! wakati wa kusemezana na D.C. neno lake ni "Ndiyo Bwana Mkubwa" ingawa hakuelewa; D.C. asemavyo yeye ni kuitikia tu. Basi ni dhahiri hakuna maendeleo yatakayotokea katika Usambaa kwamba viongozi ni watu wasio elimu.

Tazameni hilo: mabwana D.C. wetu hujibidiisha sana kuendesha kila jambo lakini hakuna anayewatia shime. Unaweza kutembea maili nyingi bila ya kukuta hospitali wala skuli. Jambo kubwa sana ni kukomesha utawala huo wa Wakilindi.

Tunaomba ukomeshwe utawala wa Kikilindi, ili iwe kuchagua kila mtu mwenye elima ya kutosha wa ukoo wo wote hata kama fukara maadam amesoma vizuri. Tena tungewekewa President badala ya Masultani nchi yetu isitawi kwa elimu na kila jambo. Vijana mliotoka jeshini mlioko nyumbani pia shime tuitetee nchi yetu kwa kila jambo.

Footnote 103, p.127, *Mambo Leo*, Letter Hamisi M. Mtengeti, January 1947, p.1.

Maneno ya N/42663 Sgnmn H.K. Salim yaliyomo uk/110/1946 yanatiliwa nguvu na kila Mwafrika aliyeelimika. Chifu akikosa elimu ni kama mzigo juu ya raia anaowatawala, badala ya kuwa msaada juu yao – na mara nyingi raia hupata adha nyingi – kama nchi moja huko Tanga Province hivi karibuni.

Footnote 104, p.127, *Mambo Leo*, Letter Mr N.A. Nyello, March 1947, p.25.

Maneno ya … H.K. Salim yamo mioyoni mwa kila Msambaa po pote alipo. Mungu Mwenyezi amemfanya bwana huyo awe ufunguo wa kulifungua kasha la mioyo ya Wasambaa wote wa leo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aiamshe Serikali yetu tukufu isifanye ajizi kwa kulihimizia jambo hilo. Wamo Wasambaa walioelimika, wenye mioyo na nia ya kutaka kuitukuza nchi yao kwa maendeleo yafaayo.

Mkilindi kuzidi kukaa kama hivi siku hizi ni mzigo unaowalemea mno raia Wasambaa. Chief Mkilindi hutazama mshahara wake mwisho wa mwezi tu wala hafikiri juu ya kuinua raia. Maadam kashiba basi yatosha. Chief Mkilindi hupenda kujichukulia wanawake wengi tu, hata mashauri katika Native Court kwa mintarafu ya mambo ya wanawake, raia hapati haki sababa ya kupendwa mwanamke yule aolewe na [illegible]

Chief Mkilindi huwa na wanawake 10 hata zaidi. Kila mmoja ana watoto 6. Rushwa itampitaje jumbe ama chief mwenye umati kama huo niliotaja? Mtoto wa chief hupoteza maisha yake nyumbani kutarajia kuamkiwa kwa jina la Shekulwavu ama Shekumkali, hii wenyewe huona yatosha.

Chief Mkilindi afanya kazi ajifanyie yeye na wanawe. Maombi yetu kwa Serikali twaomba kwa sauti kuu, ifanye mabadiliko ya Kuchagua watu bora ikiwa Mkilindi ama Msambaa bora mwenye elimu watawale Usambaa. Wapo wengi wafanyao kazi za Serikali mbali mbali waliosoma vema, Serikali iwaalike hao waisaidie nchi yao.

Wakubwa wa Tanganyika wenye mamlaka ya Usambaa kwa uwezo wa Mungu, tuondoleeni mzigo mzito unaotulemea.

Footnote 107, p. 127, *Mambo Leo*, Letter S.Sefu Buramo, July 1945, p.81.

Ninaomba wasomaji wanifahamishe kabila hili la Wamanyema lilikotoka na asili ya kuingia Tanganyika. Walikuja kwa kupigana au vipi? Kuna wengi husikia wanaitwa Wamanyema tena hujiita Arabia-Congo, imekuwaje? Sifa zao nzuri ni kuwa ni watu wenye umoja. Watu hawa wamezagaa Tanganyika yote na Zanzibar hata Mombasa. Tena kweli Wamanyema ni watu wenye nafasi nzuri na kujisaidia hasa Dar es Salaam. Imepatikanije wao kuitwa Arabia Congo?

Footnote 146, p.134, *Mambo Leo*, Letter F.K. Karatta, September 1946, p.97.

Neno kubwa tulizingatie, kujua kama Mungu hakuwa mjinga wala si mjinga kututofautisha rangi, akatupa roho na mwili mmoja ila karama mbalimbali.

Footnote 150, p.135, *Mambo Leo*, Letter S.M. Mtengeti, August 1946, p.86.

Tena basi matokeo yenu watu wa namna hiyo si mazuri, maana hutuzalia watoto ambao mara nyingi huleta migogoro kwa kutambulikanakabila zao, yaani ukiwaweka katika utu weusi hawapo, wala katika Uzungu au Uhindi au Uarabu hawamo, huwa kama popo tu. Basi bibi maadam u mwana nchi, wataka kuvunja nchi.

Footnote 174, p.140, *Mambo Leo*, Letter Samwil D. Kiama, April 1945, p.46.

Ni heri kuolewa na mume wa taifa lako na kukaa ili kuongeza hesabu ya Waafrika, kuliko kuolewa na mgeni na kuzaa mtoto wa kishenzi ambaye atakuwa chotara, mchanganyiko wa rangi. Twapata fadhaa nyingi sana mioyoni tusikiapo kwamba fulani na fulani wameolewa au wamepanga na watu weupe.

Footnote 175, p.140, *Mambo Leo*, Letter Aaron M. Mzoo, January 1946, p.2.

Kwa maneno yako unawakataza jamaa wasio na nafasi ya fedha, wasioe; kwani hawataweza kumiliki mahitaji ya wake zao. Unawafurahia wale jamaa wanaotutia aibu na kuharibu taifa letu.

Footnote 176, p.141, *Mambo Leo*, Letter Reader A. Ramsay Mwamanda, September 1945, p.106.

Kina dada wangeweza kuyapima hayo wasingeweza kukubali kukaa na mbegu nyeupe, lakini kwa sababu ya mali, aibu hiyo hawaioni kuwa kitu.

Footnote 177, p.141, *Mambo Leo*, Letter Aaron M. Mzoo, January 1946, p.2.

Ustaarabu na furaha hailetwi na tamaa ya fedha, tamaa hiyo ya anasa ndio adui wa wema na ustaarbu wote. Ni aibu mtuleteayo dada weusi mtembeapo na weupe kama ulivyosema... Kwa vile ulivyogusa mambo ya dini – hivyo nathubutu kukuambia ya kwamba katika chuo imeandikwa, Itamfaida mtu nini kuupata ulimwengu wote akapata hasara ya roho yake?

Footnote 179, p.141, *Mambo Leo*, Letter Dvr. G.E. Naftal, December 1945, p.142.

Wako watu wengi sana huku Afrika wa mataifa mbalimbali wanaofanya maskani mwao humu, na mataifa hayo yote wako wengi waliooa watoto wetu wa Kiafrika, hali hutudharau badaa ya raha. Kwa nini mataifa mengine huoa kwetu, nasi hupewa amri kuwa hatuna ruksa kuoa mwanamke wa taifa jingine? Twaomba liwepo tangazo kuwa hakuna ruksa mweupe ye yote kuoa mweusi, na hakuna ruksa mweusi kuoa mweupe. Nchi hizi tulimo kuna amri kuwa hakuna ruksa mwanamke ye yote kuonekana ana Mwafrika, hakuna ruksa kusema na Waafrika na kama akionekana anasema nasi lazima atafungwa ingawa ua mwanamke. Je kwa nini wanawake wa Kiafrika hupenda wenye fedha zaidi ya taifa lenu?

Footnote 180, p.142, *Mambo Leo*, Letter Reader A. Ramsay Mwamanda, September 1945, p.106.

Tunaye dada mmoja Mwafrika wa papa hapa anayekaa na Mhindi. Siku moja huyo Mhindi aliarifiwa kuwa watafika wageni kwake kupumzika kwa muda wa siku chache. Basi siku ya hao wageni wake kutelemka stesheni, yule dada aliambiwa aondoke kwanza akakae kwa jamaa mmoja mtu mweusi. Mhindi aliogopa ndugu wageni wake wasije wakamfanyia matata na kumfukuza. Nilipoona hayo nikakumbuka maneno ya S.S. Mhuza wa E.A.A.R.I. Amani na K.S.J. Mbalamiuwe wa Kwa Mtoro kuwas mweusi kukaa na mweupe ni aibu*. Dada anapokaa na Mhindi hajidhani kama boi ni bora kuliko yeye, yeye anajihesabu ni bibi wa Mhindi. Lakini kwwli ni hii, boi ni bora wala hukuondoka siku ile, ndiye aliyefanya shuguli zote juu ya wageni wale.*

Footnote 181, p.142, Letter K.S.J. Mbalaminwe, July 1945, p.81.

Maneno ya Bwana Samwil D. Kiama... ni ya kweli; wapendao kuolewa au kukaa na mbegu nyeupe ni aibu. Kwanza kuzaa watoto wasio Waafrika; pili, yeye dada mwenyewe hukaa utumwani bila kujijua.

Footnote 185, p.143, *Mambo Leo*, Letter S.S. Mhuza, February 1945, p.22.

Utii ni shina la ustaarabu, nao huleta amani nyingi.

Footnote 186, p.143, *Mambo Leo*, Letter *Mzee* Waziri, May 1945, p.58.

Bwana Handhuruni Saburi kuomba uhakikisho wa magazeti ya Kizungu ni kupotea. Si haki kwa Mwafrika kuiga yote ayatendayo Mzungu. Tunaishi chini ya mbingu na mawingu katika kusaidiana, si kusaidiwa na kuegemea wengineo. Ninakiri kuwa Wazungu ni walimu wetu, bali najidai kuwa hata sisi tunayo mengi ya kuwafundisha Wazungu.

Footnote 201, p.148, *Mambo Leo*, Letter Simeon Mbaruku Muya, July 1946, p.74.

Ustaarabu wetu sisi Waafrika kwa karne yetu ya kisasa (ya Kizungu) wengine wetu wanadhani ntapatikana kwa kudai mambo ya kufanyiwa na Serikali au vyama vya kazi fulani. Kuomba mishahara mikubwa kuomba mazao yetu yauzwe kwa bei kubwa, kudai watumishi wajengewe nyumba kubwa safi za makao yao kazini; kudai mashule yaongezwe, hospitali ziongezwe, barabara na reli ziongezwe kudai watetezi wa kutetea mahitaji yetu waongezwe, kudai tupewe mamlaka ya kujitawala sisi

wenyewe, na zaidi ya yote wengine hudhani Serikali haitutendei vyema kwa maisha kwa hiyo wengine hudhani ni bora kufunga safari kwamba kutoa mahitaji yetu kwa wakuu wa koloni zetu.

Hayo yote yanatamkwa kwa tamaa tu ya juujuu siyo na msingi wo wote, kwani kuombaomba kufanyiwa mambo si msingi. Kwa mfano watu wa Ulaya kama wangehudumu kuombaomba mahitaji yao kwa walimu wao Warumi, mpaka leo wangekuwa chini kabisa. Wao walitia misingi ta matendo. Walijitoa kujijengea majumba yao ya fahari, wakalima mashamba bora, wakajitahidi kwa matendo yao, mwisho ndipo wakapata maisha haya ya ustaarabu huu walio nao hivi sasa.

Kwa hiyo mabwana na mabibi wa bara letu la Afrika, jueni sana ya kuwa ustaarabu wetu msingi wake ni kujitoa kwa kiume kufanya mambo yetu hasa kupanua mipaka ya mashamba yetu. Kupanda mimea ya vyakula vyetu na ya biashara. Masoko yetu yajae aina ya vyakula mbali mbali. Wakulima wetu mpaka watakapofika wakati huo fedha zitapatikana kuwa tele katika bara yetu, ndipo kutenda au kutendewa kwa upesi bila kuombaomba kwa maneno matupu. Mahitaji yetu yote yanadai gharama (fedha) na gharama hizo zote zategemea zitolewe na sisi wenyewe kwa jasho letu. Kwa sasa Serikali yalazimishwa itende mambo ya misaada kwa raia kwa njia isiyo ya haki, kwani ni lazima ijipatie fedha kwa kukopa kwa mifuko ya raia wa nchi nyingine, hayo si haki Mwafrika siye maskini (anajiweza). Basi waungwana jueni ya kuwa kazi za vilimo vyetu tusipoziendesha vyema hatuna maendeleo yo yote. Njaa zitatukaza mwaka kwa mwaka, madeni ya vyakula (bills) kwa Wahindi na Washihiri yatatufilisi kabisa. Watu wengi wa nchi yetu watakuwa maharamia na wakupuzi. Umalaya utazidi kuliko ulivyo sasa. Kwa hiyo maneno ya kudaidai yaachwe. Kilimo chetu na kazi zetu ndizo zitakazotupatia ustaarabu wa kweli, kila hitaji letu tutaweza kulitenda au kutendewa bila kelele yo yote.

Footnote 214, p.152, *Baraza*, Letter R.H. Howieson, 7th September 1946, p.2.

Mimi mara nyingi nimesikia kuwa mwataka kuwafukuza Wahindi, je mtawafukuza kwa njia gani hata watoke katika nchi yetu ya Afrika? Mimi naona hatuwezi kwa sababu tumo usingizini bado. Kumbukeni sisi hatuna umoja wa kuweza kufanya kitu, lakini Wahindi wana umoja wa kuweza kufanya jambo. Haya ndugu zangu fanyeni umoja nasi tuwe na maduka yetu na tusinunue kitu kwa Wahindi bali tuwe tukinunua katika maduka yetu na hii ndiyo njia moja ya kuwafukuza waende kwao maana hawatakuwa na matumizi.

Mhindi akipata fedha anapeleka kwao kuinua nchi yake, nasi tukifanya hivi mtaona nchi yetu inainuka. Basi ndugu zangu vijama kwa wazee niungeni mkono tustawishe gazeti letu.

Footnote 233, p.156, *Baraza*, Letter Benjamin M. Herman, 7th September 1946, p.2.

Nipe nafasi nimuonye Mr John Kebaso kwa maneno yake aliyoandika katika "Baraza" No.359 ya 27/7/46 juu ya Wakikuyu katika nchi ya Kisii. Nasikitika sana kuona President wa Kisii Union kutoa aibu kubwa namna hiyo ndani ya gazeti. Bwana Kebaso unajidhania kuwa na akili nyingi kati ya Waafrika wa Kenya, lakini sivyo. Wewe una haraka gani? Unafikiri Wakikuyu watapeleka wapi nchi ya Kisii? Je Wakikuyu ni Wazungu au Wahindi?

Footnote 252, p.163, *Mambo Leo*, Letter C.S.M. Hamisi bin Makobe, April 1945, p.46.

Tunairudisha chini Afrika yetu kwa fitina, uchawi, kutoaminiana na kutokuwa na umoja wa kujisaidia. Basi yafaa tuyaache ndipo tutashinda vita kwa ajili ya umoja wa kusaidiana.

Footnote 264, p.168, *Mambo Leo*, Letter No.378 Cpl. Seth Mpangara, June 1946, p.61.

Wazee na vijana wa Tanganyika nzima tafadhali mtuamue, tujue ya kweli. Kabila gani lililo kubwa katika Tanganyika Territory nzima? Ajuaye atueleze kwa utaratibu ukubwa wa kabila hilo na lilipotokea na hata likawa kubwa.

Footnote 265, p.169, (a) *Mambo Leo*, Letter Peter M. Joseph, March 1946, p.26.

Mungu amekupa akili na nguvu na mikono ili uzitumie. Ni juu yako kufanya awezavyo ili kuistaarabishi nchi yako Tanganyika.

(b) *Mambo Leo*, Letter F.K. Karatta, September 1946, p.97.

Na mwisho wa habari hii ni kutukanisha wazee waliotuzaa au kumkufuru Mungu

...

Acheni kelele tusikilize mashujaa wanaofikiri njia mojawapo ya kutuamsha sisi wa Tanganyika, watie mikono gazetini ili Chief Abidel Shangali naye yamtie wasiwasi kwenye mkutano mkubwa Legislative Council*.*

Footnote 266, p.170, *Mambo Leo*, Letter M.K.E. Baji, August 1946, p.86.

Basi usiwe na haja ya kubishana na kulaumiana na vijana gazetini, ni heri uende huko Nigeria kuliko kuchafua mawazo ya watu wafikirio mambo yenye maana ya kuweza kuinua nchi yetu Tanganyika.

Gazeti letu halikuwekwa kwa Debate *na kuandika mambo yasiyo maana, kwani mwandikapo mambo hayo ya ovyo mwafedhehesha gazeti letu kwa wageni na wengi watatuona sisi watu wa Tanganyika tungali gizani.*

Footnote 268, p.170, *Mambo Leo*, Letter A.O. Wage, October 1945, p.118.

Mara kwa mara vijana walisoma hupenda kuzungumza wakisema kuwa, Sisi watu tukaao Tanganyika hatuwezi kuendelea katika njia ya ustaarabu mpaka robo tatu za watu wajue kusema Kiingereza nao wawe wanafanya kazi ya ukarani kwa Serikali. Lakini hii siyo njia. Nchi yetu ya Tanganyika yaweza kuinuka mara moja, ikiwa vijana baada ya kwisha kuhitimu mashuleni wadharau kabisa kazi ya kutumwa, washirikiane katika kazi ya ukulima. Mtu ukiisha kuhitimu shuleni, utakuwa na maarifa yatakayoweza kukuanzishia msingi wa kazi hii ya ukulima au mtu kunfanya kazi yako mwenyewe nyingineyo. Basi huko ndiko kuiinua nchi. Mwanzo waweza kupatikana kama tukishirikiana na wakuu wetu wa vyama vya African Association, ambavyo viko kila mahali siku hizi. Yafaa tuamke na tuuanze mwanzo ili watoto wetu wasije kuwa wajinga. Mwenye kilimilimi atokee kama hivi siyvo.

Footnote 269, p.170, *Mambo Leo*, Letter M. 6749 T. Up. Simbanimoto, March 1946, p.25.

Ninamwunga mono TML 86250 W.O. II S. Chamungu Jacob kwa maneno yake katika Mambo Leo ya Oktoba 1945 uk 117. Wazo lile limeshtua mioyo ya askari maelfu tuliomo ugenini, pia hao

waliopo huku majumbani. Mungu ambaye ametutuma ugenini ndiye pekee wa kukumbukwa daima. Askari wa pande mbalimbali za Tanganyika wanaonekana pote ugenini wakihakikisha na kushuhudia hali na tabia na ustaarabu wa nchi na makabila mbalimbali ambalo ni DENI TUNALO DAIMA. Furaha gani ingekuwa kama kila Mtanganyika angekuwa na nia kama hiyo yako? Shukrani gani ingekuwa kwa Watanganyika wa kesho kuona Tanganyika katika hali ya juu na njema? Mengi tuonayo huku ugenini hakika yangekuwa ni "mbolea njema" katika T.T. kama kile mmoja wetu atanuia kuichukua na kuimwaga katika (Bustani) T.T.

Footnote 270, p.170, *Mambo Leo*, Letter I. Selemani and M.A. Max, June 1946, p.61.

Watu wa kiume wa Tanganyika ni wapesi sana kuingia mkondo wa ustaarabu kuliko wanawake wa Tanganyika. Wanawake wa Tanganyika hawapati elimu kama ya wanaume, na kosa kubwa sana laandamana na wanaume wenyewe. Wanaume kwa shida kadha wa kadha hawana au wanao uwezo mdogo sana wa kuwaelimisha wanawake walio katika mamlaka yao. Kwa yakini ustaarabu wa Kizungu ni bora kwa sababu ustaarabu huo uko pande zote: kwa waume na wake. Ustaarabu wa Waarabu ni kwa waume tu; kwa wake, huwa haiwezekani kuhudhuria mbele ya wanaume wawili au watatu. Hilo ndilo jambo tulilolifuata sana likatucheleweshe zaidi katika maendeleo yetu. Sisi wote tunafahamu ya kuwa, jamaa wa kiume si wote waliojaliwa kusoma, ambao wana ustaarabu wa maendeleo mema ya baadaye kuliko wanawake. Basi jamaa hao wanaume wasiosoma wanapata sehemu fulani ya elimu kwa kukaa pamoja na watu walio mbele zaidi kwa ustaarabu kama Wazungu, Waasia na wazazi wa Afrika waliosoma na wenye elimu. Kwa njia hii hupata miangaza fulani ya mambo yafaayo katika dunia hii ya leo. Pengine wanaungana na jamaa wa klabu fulani zilizomo katika miji kadha wa kadha humu Tanganyika. Humo wanapata kupambana na njia nyingi za maana, kama kufahamu mambo ya magatezini na kusomwea vitabu na jinsi. Serikali inavyoendesha sheria fulani za Tanganyika. Pengine wanapata kujua hali ya mvua za nchi ngyingine na mengi zaidi. Pia wanapata kuzoea na kuelewa jinsi ya kutumia ubongo katika hoja na kujibu jambo kwa fikira barabara.

Hakuna watu tunaowakubali kuwa ni wastaarabu kuliko Wazungu, basi ni dhahiri kabisa kuwa mwendo wa ustaarabu ni kuiga yayo hayo ya hao walio wastaarabu tunaowakubali. Tusipokubali kuwaiga basi yonyesha hatutaki ustaarabu. Tazama tunapenda kushirikiana na mabibi wa kikwetu (Tanganyika) katika mambo ya upuzi kama vile ngoma, kulewa pombe na mengine mengi. Haya! ni aibu gani wao kuhudhuria katika mabaraza (Meetings) na Clubs; ili nao waone na kusikia tunayofanya na kuyasema.

Tukiwa nao, mwisho kati yao tutawapata wengine watakaokuwa ni viongozi has baadaye. Jambo la kutoshirikiana na wake zetu kwa mambo kama haya ni sawa na mtu aliyevaa nguo safi na hali mwili wake ni mchafu. Kwa kuipenda nchi yangu na jamaa zangu wa Tanganyika kwa maendeleo mema ninawashauri kwamba tushirikiane na wake zetu kwa mwendo wa ustaarabu tangu leo, ili tuondoe kiza na ukungu unaowaziba watu wa uani.

Footnote 271, p.171, *Mambo Leo*, Letter 44460 Sgt. Kheri Rashidi, July 1946, p.74.

Kila mtu wa Tanganyika anafahamu kwamba Umoja ni nguvu, lakini watu hawapendi kufikiri umoja huu tutauanzaje. Ni juu ya watu wote waliokarimiwa elimu kuwaongoza wenzi wao. Kuna tofauti nygingi sana za watu, basi wasipoongozwa hawawezi kutenda jambo ingawa wanalijua. Basi hayo yote yanategemea hao waliokarimiwa akili: na bila ya umoja hatuwezi kuendelea nchi hii ya

Tanganyika hata kidogo. Tushikane ndipo tuiinue nchi yetu. Niungeni mkono. Kucheza dansi tu si ustaarabu ukiwa bado hujui kujiongoza mwenyewe.

Footnote 272, p.171, *Mambo Leo*, Letter AC/20116 RSM Peter M. Joseph, March 1946, p.26.

Nchi za wastaarabu hufanya kazi mume kwa mke wajipatie riziki zao bibi na bwana. Huku tunao askari wanawake wa kila kabila, elfu elfu. Nao wanawake wa kiraia wanafanya kazi nzito za P.W.D. na kadhalika. Mabibi hawa wamestaarabika kwa kiasi chao, nao wanao mabwana; lakini wanafanya kazi hizi nzito kwa ajili ya kutaka kuendesha na kuiinua nchi yao zaidi na kujipatia nguo, chakula na vitanda maridadi kwa mali wapatayo kwa jasho lao. Mungu amesema kuwa: "Kila Binadamu atapata riziki kwa jasho yake." *Vyo vyasema,* "Afadhali kufa kwa dhiki kuliko kula senti moja ya kutoka dhambini." *Ustaarabu hauji tu kwa kulala na kupata mali bure, au mali ya kutoka katika njia za madhambi kama hizo ulizozitaja katika gazeti. Mungu amekupa akili na nguvu na mikono ili uzitumie. Ni juu yako kufanya uwezavyo ili kuistaarabisha nchi yako Tanganyika. Kama ungalivuka huku ng'ambo na kuona aibu zote za hao weupe unaowapenda kwa ajili ya kukupa kitanda safi na chakula kizuri na kukashifu taifa lako, nadhani ungalitapika na kuipenda sana rangi yako na taifa lako.*

Chapter Three

Footnote 4, p.179, *Mwafrika*, Letter Shabani Shimbo, 18th October 1958, p.2.

Bwana Mtengenezaji, hebu niwaulize hao wakuu wa shangwe hii kwamba: hii ndio kusema hapakuwa na Mwafrika hata mmoja amabye angestahili kula meza moja na hao wazungu na Wahindi? Au nyie mnapendelea Ubaguzi wa rangi udumu humu nchini mwetu milele na milele?

Footnote 28, p.184, *Mwafrika*, 19th December 1959, p.4.

Tanganyika imefanikiwa kufikia hatua hii ya leo kwa sababu haikujali ubaguzi wa rangi au taifa. Watu wake hawakujali mambo mengine ila kuwaona wote kuwa ni viumbe walio na haki sawa mbele ya Mungu.

Footnote 32, p.185, *Mwafrika*, 9th August 1958, p.3.

"Afrika iliumbwa kwa Waafrika", alisema Bibi Titi, na ni lazima Ulimwengu utambulishwe hivyo. Tokea zamani Baba zetu walikataa na kulani kabisa kutawaliwa katika nchi hii nao japokuwa walikuwa hawajuwi maarifa ya kujenga taifa lao na kutumia silaha tuzitumiazo sisi ili kuondoa fedheha hii ya Kutawaliwa bali walikuwa radhi kutumia silaha zao dhaifu na kujisalimisha kutoa maisha yao ili kuwaonyesha "Wapendao Kutawala" kuwa hawaridhiki hata kidogo na fedheha hiyo.

Footnote 34, p.185, *Kiongozi*, Letter Balthazar Masalu, 1st October 1958, p.2.

Kutambua heshima ya asili na haki zilizo sawa na zisizonyanganyika za binadamu wote, ndiyo msingi wa uhuru, na ni haki na amani duniani.

Footnote 37, p.186, *Mwafrika*, 19th December 1959, p.4.

Katika hali ya uchumi Bwana Nyerere alisema kuwa Tanganyika kwa bahati mbaya utajiri uko katika mikono ya mataifa ya kigeni na umaskini uko mikononi mwa Waafrika.

Footnote 40, p.187, *Mwafrika*, 23rd August 1958, p.5.

Lakini kabla sijasahau hebu niwape tafsiri ya usemi wa Robert Edwards kama ulivyochukuliwa katika 'Kenya Comment' ya tarehe 8/8/58. Alikuwa akizungumza juu ya hatari ya Ukomunisti katika Afrika na mtasikia faida ya makoloni kutoka kinywani mwa watawala wetu:-

"..... Inapita kando ya jangwa la Sahara ambako Wafaransa wanatumainia kupata mafuta yote (Petroli n.k.) wanayohitaji.

"Anayetawala huwa na sauti katika Afrika nzima – pamoja na mashimo ya shaba ya Rhodesia asili ya 'dollar' (pesa za Kiamerika ambazo lazima zitumiwe wakati wa kununua bidhaa za Kiamerika) nyingi za Uingereza.

"Kuwait..... ndio asili kubwa ya oili na petroli. Bila nchi hii viwada vyetu vingi vitasimama, na mamilioni ya wafanya kazi wataishi kimaskini. Petroli.... haitatosha hata kwa kazi muhimu.

"Kupotelewa na Kuwait kutakuwa kukubwa kuliko hasara iwezayo kuangukia Uingereza wakati wa vita.

"Afadhali kufa tukitetea mali yetu kuliko kufa kifo kibaya cha taratibu kwa njaa, na huku mikono ya mahasidi ikitukaba shingo."

Sikuongeza lolote. Hebu soma tena na utafakuri maneno ya mzungu huyu halafu utona kwa nini "Bado hujawa tayari kujitawala." Halafu utaona kwa nini "Nchi yako maskini." Halafu utaona kwa nini "Mnafukuza fedha za kigeni." Kama kwamba alitoea usemi wangu wa wiki jana kwamba sababu za kutawaliwa zikilinganishwa ni zile zile za nama hizo.

Sasa na turudie kwenye gumzo letu la wiki hii; Kutafuta masoko ya vitu viundwavyo Ulaya. Tufanye mathalani, fundi anatengeneza kiti kiwandani kwake. Tumaini lake ni kwamba atapata mnunuzi. Akikosa mnunuzi huwa amepoteza mbao, misumari, nguvu zake, ufundi wake, na labda hata kodi ya kiwanda. Kwa hiyo ni lazima apate mnunuzi. Na kama akipata watu wanaonunua kwake siku zote si heri kwake? Hivyo basi iliwalazimu wazungu watafute masoko ya bidhaa zao. Nilieleza hapa kwanza kwamba makoloni yalianza kutafutwa kwa makini sana wakati wa uvumbuzi wa mashine. Mashine hizo ziliunda vitu vingi vya kutosheleza nchi yenyewe na kubakiza sana. Sasa basi, Mwingereza hawezi kumwuzia Mfaransa na yeye anatafuta pa kuuzia. Waende wapi basi? Katika makoloni. Huko watu hawajui kuunda basikeli, hawajui kutengeneza nguo, hawajui kuunda sahani za chuma, na k.w.k. Basi wote walimiminika sokoni Afrika, kama vile madereva wa taxi wanvyochomoka meli ikiingia bandarini.

Ilikuwa pata shika hapa Afrika, na kila taifa la Ulaya lilitaka kuilinda sehemu yake lisije likanyang'anywa na wanunuzi wengine. Njia mbili zilitumiwa kuyalinda masoko:

1. *Walowezi (Settlers) watiwala sehemu hiyo ya nchi na kuwalazimisha wananchi kununua mali ya nchi yao tu.*

2. *Waliyazuia mataifa mengine yasiuze chocote nchini ama kwa kukataza tu ama kwa kuzitoza bidhaa za wenzao ushuru mkali.*

   Kwa hiyo ukitaka usitake, yote ni mamoja. Utanunua mali ya watawala wako tu. Kikiwa ghali au rahisi; kikiwa kibovu au madhubuti; kikiwa maridadi au basi tu. Mpango huu huitwa "Kulinda Biashara" (Protective tariffs). Kichekesho ni kwamba hapa Tanganyika tunayo sheria inayolinda vitu vinavyoundwa nchini humu visijeondolewa sokoni na mali ya kigeni.

   ...

Ikiwa kama hujaamini kuwa Serikali zetu ni serikalu za biashara kumbuka kwama Nigeria ilitawala na Royal Niger Company kabla ya Serikali ya Uingereza kuingia. Vivyo hivyo British East Afrika Company katika Afrika Mashariki na Kampuni ya Cecil Rhodes katika Afrika ya Kati. Nionavyo mimi Serikalu ilikuja kuwalinda Wafanyi biashara wake tu, sio kutufundisha mimi na wewe kujitawala hata kidogo.

Footnote 41, p.187, *Mwafrika*, 1st June 1958, p.5.

Sisi wote tunajua kuwa Mwingereza yupo hapa kwetu kwa sababu ya kutunyonya damu na kujipatia manufaa yake mwenyewe, na wala asitudanganye kwamba yupo hapa kwakuwa anatuonea huruma na kutaka kutufundisha ustaarabu au kuleta maendeleo ya nchi.

Footnote 42, p.187, *Mwafrika*, 23rd August 1958, p.5.

Na dawa ya haya yote, kama nionavyo mimi ni UHURU.

Footnote 43, p.188, *Mwafrika*, 1st June 1958, p.5.

"Hakuna njia ya kutimiza jambo hili ila ni kwa wananchi kukamata madaraka ya nchi yao, kupata uhuru na kujitawala wenyewe. Uhuru ndio unfunguo utakao ondoa vipingamizi vya utaajiri na kuleta maendeleo." (Dr. Kwame Nkrumah katika kitabu chake Towards Colonial Freedom.)

Footnote 46, p.188, *Mwafrika*, Letter A. Willy, 30th May 1959, p.2.

Naomba nafasi katika gazeti lako ili nitoe maoni yangu juu ya umaskini wa nchi ya Tanagnyika, kwa kweli sioni sababu yoyote iliyomfanya Waziri wa fedha atamke kuwa Tanganyika ni masikini. Mimi sikubaliani nao hata kidogo nikikumbuka kuwa, kuna nafaka nyingi mno pamoja na madini kadha wa kadha ambayo mpaka wakati huu yanabugujika kwa wingi sana humu nchini, na hivi ndivyo vitu halisi viletavyo utajiri wa nchi tu.

Mara kwa mara tunaambiwa kuwa, sisi tunapata misaada mingi kutoka Uingereza. Ningependa kufahamu kuwa Uingereza hupata wapi fedha za kuwakopesha Wananchi katika nchi za nje? Hii ni kwa ajili ya mazao yetu ambayo bei yake hukadiriwa Uingereza mara kwa mara, nayo hununuliwa kwa bei ya chini sana, na halafu huenda kuuzwa kwa bei ya juu sana ndivyo basi sisi daima huachwa masikini.

Footnote 47, p.188, *Mwafrika*, Letter M.A. Mbunda, 9th September 1961, p.21.

Kote nchini wanashirikiana bega kwa bega, ili kuwatosa maadui watatu, ujinga, umaskini na ungonjwa. Ukitazama sana, utaona kwamba wananchi wameanza kupata taabu tangu mataifa ya kigeni yalipoanza kuingia katika kontinenti la Afrika. Hawa wengi wamekuwa magugu katika shamba – 'Afrika', na kuwaharibu wananchi kwa kuwanyima chakula ambacho ni haki yao nao wanakila chote hata wananchi wanaambiwa ni maskini.

Afrika si maskini hata kidogo. Kuna mali sawa katika nchi hii ambayo imeshikwa na hawa wageni. Je, ni lini watatuachia mali hizo, kama vile madini na ardhi yenyewe. Mimi nafikiri itabidi tuwang'owe kama tunavyoyang'oa magugu katika mashamba.

Wahindi wanapotoka India huwa hawana chao, lakini baada ya miaka michache utawaona wana nyumba, maduka na kadhalika. Waarabu nao kadhalika.

Waingereza wanapofika ni lugha tu wanayotuletea, fedha hawana. Lakini wakija hujipangia mishahara minene na kumsahau mwananchi. Baada ya miaka michache huwa matajiri wa kutosha.

Footnote 48, p.189, *Mwafrika*, Letter *Bi*. Joice Kilabaka, 25th April 1959, p.2.

Mara kwa mara hali ya nyumba za Wazungu, na Wahindi ambao huwa wa meajiriwa pamoja na Waafrika katika kazi moja, nuimba zao hao wageni, huwa zimejengwa imara sana na madhubuti;

hupakwa chokaa nje na ndani, na sakafu rasmini. Lakini nyumba za Wafrika huwa mara kwa mara katika hali mbaya sana, nyumba hizi huvuja; huwa zina chumba kimoja tu. Mimi daima hushangazawa sana na jambo hili hasa nikikumbuka kuwa ardhi hii ni mali yetu wenyewe.

Kwa maoni yangu ningalipendelea kuona kuwa Wazungu na Wahindi wangalikalia zile nyumba ambazo Waafrika wanazikalia kwa sasa nasi tukalie xile ambazo wao wanazikalia kwa wakati huu ili mradi tuweze kuzilipa ikiwa ni lazima. Tu tayari kabisa nasi kukaa mahumba mabovu tukiwa India, na Ulaya. Lakini inasikitisha sana kumwona Mwafrika akihangaikia numba katika nchi yake mwenyewe.

Lakini ninaamini kabisa kuwa yatamalizika kabisa mara tu baada ya nchi hii kujipatia uhuru wake.

Footnote 49, p.189, *Kiongozi*, Letter Charles N. Kamata, 1st April 1958, p.2.

Je, enyi wenzangu mwajua kuwa kutawaliwa ni kubaya, na ikiwa mwajua hivyo ni nafasi yenu kumwomba Mwingereza uhuru wetu?

Footnote 50, p.189, *Mwafrika* Letter K. Philipos, 2nd May 1959, p.2.

Ni jambo la kusikitisha mno kwamba ndugu zetu hawa hawakumbuki udhalimu unaopitishwa na utawala huu wa kigeni, pia hawafikirii uchochezi unaofanywa na wageni hawa kusudi kuharibu amani na uhusiano mwema usiwepo humu nchini, uhusiano ambao Wananchi kwa jumla wameungana na kujibadhi katika chama maalum yaani TANU.

Mfano bora ninaotaka kuwatolea na ambao no wajibu wao kuufuata, ni ule Mkutano mkuu wa Machifu uliofanyika hivi karibuni huko Tabora. Mfano huu nimaamini utakuwa ni mafundisho bora sana katika hao jamaa ambao mioyo yao daima ilikuwa haina mapenzi na madai ya TANU. Nawaomba pia watawala wetu wa jimbo la Ziwa waunganike haraka katika kuutafuta UHURU wakiwa pamoja nasi Wananchi.

Footnote 51, p.189, *Kiongozi*, Letter A.M.P. Tibenderana, 15th August 1959, p.3.

Watu wengi wanasema eti ingawa hatujapata uhuru wetu, lakini hiyo si sababu ya kutuzuia kumheshimu zaidi Mheshimwa Nyerere. Hata mpaka sasa anastahili heshima kubwa kwa mambo ambayo ametutendea. Hasa kumfanya kila Mwafrika afahamu kwamba kutawaliwa ni jambo bayo.

Footnote 52, p.189, *Mwafrika*, Letter Mwabugu Sarai, 9th May 1959, p.2.

Leo natoa shukrani ikimpasa. Mheshimiwa Bwana Nyerere na wasaidizi wake juu ya faida kubwa nilizozipata kutokana na Chama cha TANU. Kwani kabla ya Chama hiki kuzushwa ukweli ni kwamba, binafsi yanu sikuelewa wala sikufahamu nini hasara au faida ya kutawaliwa. Kifungu cha pili ambacho sikukifahamu akilini mwangu ni kwamba nilijua tu ya kama. Serikali yetu ua Kiingereza inatawala ulimwengu wote na wala sikujua hata kidogo kuwa kuna nchi nyingine zinajitawala na kujitegemea. Mpaka hapo tu kabla ya kuendelea ingempasa yeyote ambaye hakufahamikiwa kama nilivyoshindwa kufahamikiwa mimi, amwombee Dua jema Bwana Nyerere ambaye ni Nabii aliyezuka

katika Karne hii, na ambaye ndiye anayetuoka katika pango tulilotumbukizwa bila kufahamu wala kujua kitu gani kilichokuwa kikitendeka.

Ingawaje kulikuwa na watu mashuhuri toka wakati huo, labda nisingaliwalaumu watu huo kwamba hawakujaliwa kufanikiwa na hekima hizi.

Nikimaliza usemi wangu ningesema kuwa hakuna yeyote aliye binadamu na asiyejua kuwa kutawaliwa ni kubaya. Hata yule atutawalae anatambua wazi kuwa kutawaliwa ni kubaya.

Footnote 53, p.189, *Kiongozi*, 17th November 1959, p. 4.

Neno hii UHURU limevuma sana nchini, hata mbuzi na ngombe na wanyama wengineo wamelisikia wakachoka. Limeandikwa katika magazeti na kuzungumzwa katika mikutano, mitaani, [illegible] sokoni n.k. limetangazwa kwa radio hata limechuja ndani ya masikio yetu. Na itaendelea hivyo mpaka Serikali ya Kiingereza itakapotupa tunalotamani wote, yaani UHURU.

Footnote 57, p.192, *Kiongozi*, Letter Yeronimo John, August 1956, p.4.

Naam, Bwana Hababkuk, hakika wewe u Mnyamwezi halisi, pia unapenda kabila lako na lugha yako ya Kinyamwezi pia. Wewe umeona hatari inayoielemea lugha yetu ya Kinyamwezi, yaani imo katika njia ya kupotea na kusahaulika. Kwa kutakakuihifadhi lugha hii, umeona vema sisi Wanyamwezi tufanye mchango kusudi nasi tupate gazeti letu la lugha ya Kinyamwezi kama vile makabila mengine. Kweli hiyo ni njia mojawapo ya kulinda ulimi wetu usipotee. Lakini Bwana Habakuk, siyo tu kupata gazeti la Kinyamwezi peke yake yatosha, la. Pia tujitahidi kupata nafasi katika mashule hasa Primary Schools ili Kinyamwezi kitumike kama lugha ya kuwafundisha watoto. Hii itakuwa njia nzuri, watoto wetu wakiisha kumaliza masomo yao ya Primary watakuwa na kumbukumbu ya lugha yao.

Footnote 58, p.192, *Mwafrika*, Letter Bi. K. Nassibu, 19th December 1959, p.2

Karibu kila kabila katika Tanganyika siku hizi lina mtawala wake. Tukichukua Jimbo la Tanga itaonekana kuwa ilikuwa ni Wabondei na Wadigo tu walikuwa hawana watawala lakini sasa Wabondei pia wamekwisha kupata chifu wao. Jee lini Wadigo watapata chifu? Labda wengine watauliza tutampataje mtawala huyo.

Kwa maoni yangu mimi ningeshauri kama kiundwe chama cha siasa cha Wadigo wote kwa jumla ambacho kingeondoa kule katengana wenyewe kwa wenyewe na baadae kipeleke maobi yake kwa serikali kuiomba unfanywe uchaguzi wa mtawala wa Digo, kama ilivyofanya Bonde Central Union.

Ni fedheha kuona kabila kubwa lililochukua sehemu kubwa ya Wilaya ya Tanga halijitambui, halina sauti, halijui hata haki zake. Kabila ambalo ni taajiri, lenye mazao ya nazi na mifugo.

Ninamalizia barua yangu kwa kuwaita wale Wadigo ambao hivi leo ni Ma A.D.O., walimu wakubwa, waganga wasitidhike na vyeo hivyo pekee, bali warudi kuja kuiamsha Digo. Kumbukeni kuwa ni Mdigo tu ambae ana haki ya utawala wa Digo.

Footnote 60, p.192, *Mwafrika*, Letter Boniface Mwakibeta, 23rd July 1960, p.2.

Itafahamika kuwa serikali za mitaa za kikoloni ziliundwa kwa mpango wa kikoloni ambao raia hawakushauriwa na kukubali lakini sasa ikiwa tunabadili serikali kuu lazima na serikali za kienyeji, ambazo ziko karibu nasi zaidi, tuzibadili.

Footnote 65, p.193, *Mwafrika*, Letter J.C. Patila, 30th May 1959, p.2.

Ili nipate kuwasaidieni kidogo katika uchaguzi wenu naomba mwepukane na mtu ye yote mwenye:-

...

(3) Asiye na elimu ye yote kwani ataweza kudanganywa kwa urahisi kadhalika hatujua afanye nini kwa kuendeleza nchi yake.

Footnote 66, p.194, *Ngurumo*, 23rd January 1961, p.1.

Maelezo ya azimio la pili juu ya Serikali ya Kienyeji mkutano ulilaumu vikali jinsi Serikali hiyo inavyoendeshwa, haiendeshwi kidemokrasi. Chifu anawapa ndugu zake kazi, hazina haingaliwi inavyopasa, cheo chake anakitumia vibaya, Uhehe anaifanya ni mali yake na kwamba ni kwa sababu yake ndio maana nchi hiyo iko nyuma katika maendeleo.

Footnote 67, p.194, *Kiongozi*, Letter Credo Punyo, 15th December 1960, p.3.

Ndugu msomaji, mtaalamu wa mawazo ya kuanzisha chama katueleza dhuluma za hawa Wanyama (Watemi). Kuwa Mwanangwa, Mkubwa wa Baraza au tarishi mpaka umridhishe Wanyama au uwe ndugu yake. Utawala wa namna hii ni utawala wa dhuluma, haki haitendeki. Kama alivyosema Bwana Matta ni wajibu wetu sisi raia wa Unyamwezi kuchagua watawala wetu badala ya Wanyama.

Kumekucha, yote wayatendayo tunayaona. Uskiu umekwisha pita, weka mchuzi kwangu kukavu au vutia kwangu ni utawala usio timiza haki za kidemokrasi. Jamaa Wanyamwezi wenye ujuzi na elimu ya kutosha nchini Unyamwezi, anzisheni chama hiki kitukufu, nasi akina Punyo tuko tayari kuwa wanachama wenu wa kwanza.

Penye haki uongo hujitenga ndugu Wanyamwezi tuungane bega kwa bega mpaka tuondoe fedheha hii. Hapa natia komeo, na nangoja wananchi wenzangu watasemaje.

Footnote 69, p.194, *Mwafrika*, Letter M. Mateso, 4th June 1960, p.2.

Watawala wa sehemu nyingi za Songea ni wale ambao wamerithi na ambao wamehimizwa kusoma na serikali ya Kiingereza, Watawala hao hata hivyo wengi wao kama si wote hawahimizi elimu. Watu wengi wenye elimu hawako katika kuendehsa kazi za utawala wa Wilaya hii.

Tawala za Wilaya hii zote ni za kizamani sana na watawala wanazidi kuzifanya zirudi nyuma tu. Wengine wakisikia habari za maendeleo kama yaliyoko Uchaggani, Buhaya, au Upare inakuwa kama wamesikia sauti sikio moja na kutokea sikio la pili.

Ingawa watu wengi wana elimu na pia kuna utajiri wa asili na wakulima wanajitahidi katika Wilaya ya Songea, lakini bado mamlaka ya serikali yako chini ya watu wachache. Wahalmashauri wa

komiti za wenyeji huchaguliwa na watawala na wala si raia. Wengi wao ni wazee wasiojua kusoma au kuandika na maendelezo yao ya mambo ya utawala ni yale kizamani. Halmashauri nyingi zinakuwa zikipinga kuchaguliwa kwa watu wa kuendesha mabaraza hayo. Hasa hawapendi kuweko kwa watu waliochaguliwa kwa kura.

Footnote 72, p.195, *Kiongozi*, Letter M.S.S. Mata, 1st November 1960, p.3.

Jinsi tunavyotawaliwa hapa Unyamwezi, sivyo tunavyotaka raia. Utawala tunaoutaka ni ule wajibu wa raia kuwachagua watawala wao badala ya "Wanyama" (Watemi).

"Wanyama" anapochagua wasaidizi wa nchi, huchagua wanaomridhisha yeye na kuwaangamiza raia. Jambo linaloleta uchungu na fedheha ni lile la kuweka Mkubwa wa Kipande, Mwanangwa, Tarishi na Wakubwa wa Mabaraza wakiwa ukoo mmoja. Je, wangepewa wajibu raia kuwachagua walinzi hao wangelichagua ukoo mmoja? Ndiyo kusema hawa wana elimu kuliko raia wengine? Ukichungua, haki haitendeki. Kwa kutolinda haki katika nchi ya Unyamwezi, kunaleta kuvunja heshima za raia. Jibu linalotolewa ni kwamba "kokote ukienda, utanikuta tu." Hapo yeye anataka lolote atakalotamka ukubali, maana nchi nzima wameikalia.

Jambo ambalo nawaomba raia ni kutengeneza kitu kimoja kitakachochungua haki na heshima ya kibinadamu. Kitu hicho kitaitwa U.D.P. yaani Unyamwezi Democratic Party. Kazi yake itakuwa kuchagua watawala kwa muda utakaokadiriwa na chama hicho. Mimi sioni haki kwa nini raia asichague watawala wake. Je, Unyamwezi tutasema iko katika utawala gani?

Footnote 73, p.195, *Kiongozi*, Letter J.K. Yakale, 15th December 1960, p.3.

Watemi kuturithi sisi raia kama vile watumwa, haifai. Raia wapewe uhuru wa kuwachagua watemi wao hata wanangwa pia.

Footnote 74, p.195, *Kiongozi*, Letter H.M. Kiswagara, 1st May 1959, p.3.

Kuna mfano mzuri sana nao ni na Wachagga. Toka Wachagga walipokuwa na Chifu mkuu, wamepata maendeleo mazuri na wamesifiwa kila mahali. Chifu wao mkuu ameiletea sifa nzuri nchi yake pamoja na Wachagga wenyewe.

Footnote 75, p.195, *Kiongozi*, Letter William Madafu, 16th March 1959, p.3.

Lingekuwa jambo la manufaa sana kwetu sisi Wanyanwezi kuungana na kuwa chini ya mkuu mmoja. Mkuu huyo asimamie kabila letu katika Wilaya za Tabora, Nzega na Kahama. Uongozi utolewe wa namna moja utakaowafaa wenyeji kwa jumla. Msingi bora wa ushirikiano uanze kujengwa na kuimarishwa, utakaokuwa mwamba baaday

...

Waungwana, "umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu." Nawaombeni nanyi wakubwa wetu hasa Watemi wa Unyamwezi yote mlichunguze vema jambo hili. Matatizo yenu nasi raia yatakomeshwa upesi.

Footnote 76, p.196, *Kiongozi*, Letter Hashim L. Ndambile, 17th January 1961, p.3.

Kufuata shabaha ya Bwana Mata, baada ya kuanzisha Chama hicho ni kuwafukuza Watemi wetu na kuwachagua Watawala wengine badala yao, ati kwa sababu utawala chini ya Watemi ni wa dhuluma. Bwana, nafikiri hukufikiri vema kufanya wazo hilo liwe ndiyo shabaha kubwa ya U.D.P. Nadhani Bwana Mata hujui historia ya Utawala wa Kienyeji unavyoendeshwa na watemi. Nitakufahamisha kuwa Watemi ni watawala wa asili na wamekuwa watawala baada ya kupigana vita kabila kwa kabila mpaka kabila moja liliposhindwa. Aliyekuwa Kiongozi wa wale walioshinda alichaguliwa kuwa mtemi wa nchi hiyo (kama ilivyo kawaida ya vita kila mahali duniani). Ndiyo maana kila mahali ukoo unaotawala ni ule ule moja tu kwa kufuata heshima hiyo.

Ningependa pia Bwana Mata usome Historia ya nchi nyingine zenye serikali ya Demokrasi. Kwa mfano Uingereza imekuwa na watawala wa asili kwa kufuata mambo hayo niliyoeleza hapo juu, na ni heshima kubwa kwa nchi kuwa na watawala wa asili na jadi kuliko kuchagua mtu ye yote tu kama vile katika mambo ya siasa.

Mimi nashauri kwamba shabaha kubwa ya U.D.P. iwe kuangalia kwamba haki katika mambo ya Utawala wa Kienyeji inafanywa kama ilivyo sheria ya Demokrasi na wala sio kuwafukuza Watemi wetu wa asili kwani hiyo ni fedheha kubwa kwa kabila letu Wanyamwezi.

Footnote 79, p.197, *Mwafrika*, 16th July 1960, p.3.

Mipango kuhusu serikali za mitaa na machifu, pila ilielezwa. Machifu watakuwapo na watakuwa na sauti katika kuendesha nchi. Lakini kufanya kazi kwao kutategemea raia wa sehemu ile walipo, kwani serikali itapendelea mambo ya wilaya yaendeshwe na wananchi watakaochaguliwa kwa hali ya kidemokrasi.

Footnote 86, p.198, *Mwafrika*, 1st June 1958, p.5.

Sisi hatuna silaha ila UMOJA.

Footnote 94, p.201, *Kiongozi*, Letter Bakari s/o Mlela, 15th March 1960, p.3.

Tafadhali niweke lau Mwishoni nitoe maoni yangu upande wa ndugu zangu hao watokao sehemu ya Bara. Wao huja huku pwani kwa ajili ya kutafuta kazi, baada ya kupata kazi huwa wanasahau kabisa kule walikotoka, na kuitwa "Walowezi".

Jambo linalosikitisha ni kwamba, unaweza kumkuta mzee fulani, unapomwuliza, je, baba ulifika lini nchi hii? Atakuambia mwaka niliofikia siukumbuki, isipokuwa nilikuja wakati wa vita kuu. Au atasema nilifika nchi wakati Reli ya Tanga-Arusha ilipokuwa inaanza; na ukimtazama hali yake aliyo nayo inasikitisha sana. Tena umwulizapo: Unafikiri lini utarudi nyumbani? Atakuambia: "Kurudi bara ni majaliwa ya Mungu."

Si hayo tu yanayoleta mashaka, bali hata wale wenyeji hawawajali wale "Walowezi." Kwa mfano unaweza kutokea msukosuko fulani kama vile kodi, basi hapo Jumbe na Tarishi wake wataongoza majumbani ya wale wageni. Katika kuzolewa kwa watu nanina hiyo utaona wageni 15

na wenyeji 3. Pili, mgeni anapopatikana na hatia na kupelekwa mbele ya Jumbe, jambo la kwanza ataulizwa: "Wewe kabila gani?" Akisema mimi Mngoni, au Mrundi, au Mgogo, au Mnyamwezi, basi utawasikia wazee wote walio pale Barazani wakicheka na kusema, "MNYIKA NI NGONGWE HALEKA KUSUNGU." maana yake Mnyika ni ngogwe haiachi uchungu hata ukitia kiungo. Basi hapa matokeo yake atapigwa faini kubwa au atiwe Gerezani miezi 6.

Ndugu zangu si ubaya kwenda nchi kigeni kutafuta kazi, lakini tukumbuke kurudi kwetu. Waswahili wanasema kuwa Simba akujuaye hakushambulii akakumaliza. Basi jamaa zangu kumbukeni makwenu.

Footnote 95 p.202, *Kiongozi*, Letter Charles Augustin, December 1957, p.2.

Ndugu zangu watu wa Kondoa Irangi hasa Wakristu, inakuwaje kuwaoza wageni ambao wanatoka mbali, na wala hamjui wanakotoka, na walikoa na mafundisho na kubatizwa? Mimi najitolea kuwapinga wageni wote ili wasizoee kuja Irangi kutafuta wachumba. Maana kati yao hawa wanakuja kuoa huku kwetu, huogopa wingi wa maharri katika nchi zao, walikotoka.

Footnote 96, p.202, *Kiongozi*, Letter L.H. Lubuva Sitakaifujo, 16th January 1958, p.2.

Warangi, watoto wenu wasiolewe na wageni, kwani ni kupoteza ukoo.

Footnote 97, p.202, *Kiongozi*, Letter Mwl. A.A. Namikowi, 1st September 1959, p.3.

Mara nyingi nawasikia watu wakijadiliana juu ya "kuona kwa makabila mbalimbali." Nipe nafasi nami nitoe mawazo yangu juu jambo hilo.

Mimi mwenyewe nisingependa kuoa mke wa kabila jingine ingawa ni Mtanganyika mwenzangu. Sababu zangu ni hizi:

1. *Sipendi watoto waitwe Machotara.*
2. *Wanawake wa Kiafrika hawana mafundisho ya kutosha kuhusu kuhesimiana katika ndoa. Kwa hivi siku ya kuudhiana, mambo yatakuwa mabaya zaidi.*
3. *Wazee wangu hawatamfurahia sana mke huyu asiyejua lugha yetu sawasawa wala mila za kabila letu. Wakati mimi nitakapofurahi na kuimba nyimbo za kikwetu ataniona kama nina kichaa.*

Sisi Wapogore tuna desturi hizi: a) Mwanamke havuti sigara. b) Mwanamke haruhisiwi kukaa juu kiti kirefu. c) Mke hawezi kuongwa na wakwe zake wala kula mbele yao mpake tumekwisha kuzaa watoto wawili au watatu.

Je, nikioa mke wa kabila jingine asiyejali desturi hiza atawezaja kupendwa na watu wa kwetu? Nadhani itakwa ni vigumu sana.

Footnote 104, p.205, *Kiongozi*, Letter F.M. Marenge, 14th June 1959, p.3.

Tanganyika ni yetu, ni nchi yetu, alitupa Mola wetu, ya nini kungoja kusukumwa na akina mjomba ndipo tufanye hidii?

Footnote 105, p.205, *Mwafrika*, Letter Saidi M. Mavuno, 25th June 1960, p.2.

Kusema kweli watu wote humu Tanganyika wameungana na kuwa taifa moja linaloitwa Watanganyika.

Footnote 106, p.205, *Kiongozi*, *Uhuru Na Haki Tu?*, 15th February, 1960, p.7.

Hapo amani atazaliwa baada ya kujenga ujitawala juu ya haki, na haki baada ya kupata nguvu na tulizo kwa mapendo kwa wenzetu kwani wote tuko binadamu, Baba yetu mmoja, Mungu, tena tuko ndugu kwa mama mmoja – TANGANYIKA.

Footnote 107, p.205, *Kiongozi*, Letter "*Mtanganyika*", March 1957, p.4.

Katika enzi ya Kidachi watu walitengana na kubaguana kwa makabila; lakini leo sisi ni Watanganyika. Sisi tu ukoo mmoja na nchi yetu ni mmoja tu: "Tanganyika".

Footnote 109, p.206, *Kiongozi*, Letter "*Mtanganyika*", March 1957, p.4.

Ewe Mtanganyika, sasa huu ndio wakati timamu wa kustawisha maendeleo ya nchi yako, kabila lako linakungoja wewe hapo.

Footnote 110, p.206, *Kiongozi*, Letter J.K. Kiimbila, 1st October 1959, p.3.

Kumbuka Mwalimu: Neno kubwa katika barua yako hukufikiria neno "Mapenzi". Umesema pia kuwa hutaki kumwoa mwanamke wa kabila jingine ati kwa sababu hupendi watoto waitwe machotara. Nini msana ya machotara mwalimu? Ninavyofahamu machotara ni watoto kati ya makabila na makabila. Haidhuru hata kama ungemwoa Mchina., ikiwa kuna upendo na mmepata watoto, hiyo ni sawadi kutoka kwa Mungu. Siasa yako mwalimu ingelikuwa "Waache waseme, watachoka".

Umeendelea kusema kuwa wazazi wako hawatamfurahia sana mke wako asiyejua lugha au mila za kabila. Msemo wako umeonyesha kuwa watamfurahia ingawa si "sana". Sasa je, ikiwa mke wa kabila lako hawamfurahii kwa sababu ya tabia yake kuwa mbaya, jambo la namna hii litakataza ndoa yenu kuwako? Tofauti iko wapi kati ya hawa wawili?

Kumbuka Yule aliyesema ya kuwa kila mmoja atamwacha baba na mama aandamane na mke wake... NAO WATAKUWA MWILI MMOJA. Na hivyo ikiwa wazee hawapendi mwili wangu, sawa tu, hawanipendi hata mimi. Kumbuka tena kutojua mila au lugha ya mwingine si neno. Katika ulimwengu wa sas watu wa makabila tofauti wanaweza kuishi pamoja kwa kuchukua desturi za kawaida ambazo hazina mapaswa kama uliyoyataja.

Mwalimu, desturi kama hizo ulizotaja katika barua yako kama kisingizio cha kutooana na makabila mbalimbali, hatuwezi kuzifuata hata kama ni za jadi, lazima tuzipige mateke, na tubakie na zile zinazofaa. Vile vile kumbuka kuwa mambo ya ukabila yamekwisha katika sehemu zingine za Tanganyika.

Footnote 111, p.207, *Kiongozi*, Letter Michael L.I., 1st May 1960, p.3.

Barua hiyo ukiisoma kwa makini utaona kuwa inaweza kuleta udanganyifu wa kutosha katika mambo fulani yaliyo muhimu kwa Watangayika. Mambo hayo ni kama haya yafuatayo:

a) *Barua hiyo inavunja amri ya mapendo yaani kumpenda jirani.*
b) *Barua hiyo inatenga na kuleta ubaguzi wa makabila ya Tanganyika, yaliyo PWANI na BARA yasichanganyikane.*
c) *Barua hiyo inaonyesha dharau na chuki ya watu wa PWANI pamoja na wazee wa mabaraza kutowathamini walowezi Waafrika wenzao ambao ni Watanganyika.*
d) *Yumkini pamoja na hayo barua inasema kwamba simba akujuaye hakushambulii akakumaliza, basi mpaka hapo barua hiyo imetuonyesha kuwa Watanganyika wa PWANI hawawajui Watanganyika wa BARA. Barua hiyo pia inamzuia Mtanganyika kwa kumnyima uhuru wake wa kuweza kukaa na kuishi kwa hiyari katika Tanganyika yake penzi, mahali ambapo hakuzaliwa katika sehemu hiyo kama PWANI.*

Footnote 112, p.207, *Kiongozi*, Letter H.H. Kalunga, 1st May 1960, p.3.

Lakini nakuomba ukumbuke kwa "Tanganyika ni kwetu" na hivyo usiwanyanyase wananchi wenzako na kuwaita "wageni" au "walowezi", kwa kuwa "wageni" ni watu waendao mahali fulani na mwisho wakichoka kukaa wanarudi kwao. Lakini hao uwasemao ni wananchi ndiyo maana hukaa popote wapapendapo. "Walowezi" ni masetla wanaotaka mbali na kukamata sehmu kubwa ya ardhi, kwa sababu wana fedha, huyafanya mashamba hayo kutwa mali yao kwa muda watakao wenyewe kwa Serikali. Kwa hiyo usimwite Mnyamwezi au Msukuma akikaa Korogwe akajenga kibanda chake cha matope, kijishamba cha maharage na kuoa Mzigua, kawa mlowezi au mgeni. Nadhani mpaka sasa unafahamu wageni au walowezi katika Tanganyika ni akina nani, kama kuwajui, basi tena!

Footnote 114, p.207, *Mwafrika*, 9th April 1960, p.6.

Laibon Merishari Oroma, mkuu wa dini wa Wamasai alikataa mbele ya umati wa watu zaidi ya 20,000 mjini Dar es Salaam kwamba Wamasai wa Tanganyika wana hamu ya kuondoka Tanganyika na kujiunga na Wamasai wa Kenya wakati nchi hii ikiwa huru.

Laibon huyu ambae alihutubia mkutano wa TANU pamoja na Bwana Nyerere alitamka kuwa Wamasai hawataki kujibagua na makabila mengine ya Tanganyika, na kwamba wanamwamini Bwana Nyerere.

Hivi karibuni ulienea uvumi eti Wamasai wa Tanganyika watajitenga. Maneno haya yalimleta Laibon Oroma mpaka Dar es Salaam kuonana na wakuu wa TANU.

Footnote 115, p.208, *Kiongozi*, 1st April 1960, p.4.

Majadiliano ambayo yameendelea katika KIONGOZI kuanzia toleo la tarehe 15 Januari mpaka toleo hili, yameleta faida kwa wasomaji wetu kwa kuwa yamewafanya wafikiri zaidi juu ya shauri hili muhimu la mahari. Shauri hili linatutalanisha siyo sisi wa humu Tanganyika peke yetu, lakini Waafrika wa nchi nyingine pia.

Fotenote 118, p.209, *Ngurumo*, 2nd December 1961, p.1.

Sheria ya uraia wa Tanganyika kidogo itawapendelea watu kutoka nchi nyingine za Kiafrika. Watu kutoka nchi nyingine za Kiafrika wataweza kuandika maombi ya uraia wa Tanganyika kwa kufuata utaratibu wa watu waliotoka kwenye nchi za Commonwealth.

Kwa njia hii raia wa nchi yo yote ya Kiafrika, unaweza kuwa raia Tanganyika kuwa urahisi zaidi kuliko wale wageni. "Na kwa kufanya hivyo atauonyesha ulimwengu kwamba Tanganyika ni nchi ya Waafrika; na kwamba tunatambua heshima za upendi kwa ndugu zetu katika nchi nyingine.

Footnote 123, p.210, *Kiongozi*, Letter "Mwenye Wasiwasi", 13th September 1960, p.3.

Kwa kuwa Bwana J.K. Nyerere amesema wazi kwamba hayo ni maoni tu, wala si lazima yatimizwe, nawaomba viongozi wa Tanu wazidi kudai kwana uhuru kamili kabla ya kuziunganisha nchi kwa sababu kizi:

1. *Uhuru ni haki yetu, kivyo tuupate wakati wowote tutakapohitaji kuupata. Afadhali mapema kuliko kuchelewa.*
2. *Umoja wetu na amani yetu zimetufanya tuwe na haki ya kuupata mapema. Aksanti Rubani wetu J.K. Nyerere kwa uongozi wako mwema.*
3. *Tungedanganyika kuwangoja watu ambao hawana umoja na ambao baadhi yao hawaheshimu amani, kwani hatujui ni lini watakuwa tayari.*
4. *Wajumbe wa U.N.O. hawakutusahau. Wamesisitiza kwamba utawala kamili usicheleweshwe kupewa Watanganyika kama tuzo la jasho la umoja na amani zao.*

Kwa mwisho nawaomba viongozi wetu wananchi waishikilie kamba kwa mikono miwili, nasi tutaivuta kwa nguvu tuwezavyo mpaka tumeupata "UHURU KAMILI MAPEMA MWAKA UJAO".

Footnote 127, p.213, *Mwafrika*, Letter R.G. Siwale, 16th June 1958, p.2.

Ikiwa Waafrika wakati wao wa kupata uhuru ukitimia ni wazi watataka kuwaajiri watu wa mataifa mengine kuwafundisha mambo yote ya ufundi na kadhalila, na kuwa kuwa waalimu hao hawatakuwa na tamaa ya kushika kila kitu cha wenyeji basi hakutakuwa na uadui wowote.

Footnote 130, p.214, (a) *Ngurumo*, 5th December 1960, p.1.

"Kule kuchagua wajumbe wa Lejiko ambao si Waafrika ni kuonyesha dhabiri kwamba hatuwezi hata kidogo kuitawala nchi yetu. Sasa tuna Serikali ya kushirikiana kwa ajili ya kudanganywa na wajomba zetu ambao no waoga, waongo na wanauza nchi hii kwa umoja wa kujenga taifa la mseto. Sisi tunataka kujenga taifa la Kiafrika na ukoloni na vibaraka wake tutawapiga teke na kuwakanyaga chini ikiwa watatupinga."

(b) Kiongozi, 17th October 1959, p.1.

Juu ya A.N.C.:

1. *A.N.C.- Kuwatayarisha Waafrika wa Tanganyika tu kujitawala.*
2. *A.N.C. – Kazi zote za maana kama D.O., A.D.O, D.C., S.D.O., A.S.D.O. na kadhalika, lazima zishikwe na wakazi Waafrika wenyewe wa Tanganyika zitakapoachwa na Watumishi wa Kiingereza (Expatriate Officers).*
3. *A.N.C. – Haiwezekani kwa wakati uliyopo Mzungu au Mhindi au Mwarabu kupewa haki ya uraia, maana Mwafrika atapoteza mengi.*
4. *A.N.C. – Ni Mwafrika tu ndiye mwenye haki ya kuchaguliwa katika Baraza la Kutunga Sheria, bali hatuna kuziwizi juu ya Mzungu, Mhindi au Mwarabu kuitumia kura ambayo ni haki yake. Kwa hiyo A.N.C. haitakuwa tayari kuwaomba wanachama wake kumchagua mgeni yeyote atakayetaka kugombea uchaguzi ujao wa Baraza la Kutunga Sheria.*

Juu ya T.A.N.U.:

1. *T.A.N.U. – Kuwatayarisha Waafrika, Wahindi, Waarabu na Wazungu wa Tanganyika kujitawala. Si Waafrika peke yao.*
2. *T.A.N.U. – Mkazi yoyote wa Tanganyika akiwa Mzungu au Mwaarabu au Mhindi anayo haki ya kupewa kazi hizo baada ya kuondoka Waingereza (Expatriate Officers).*
3. *T.A.N.U. – Inafaa haki ya raia itolewe tangu sasa kwa wakazi wote wa Tanganyika bila kujali rangi.*
4. *T.A.N.U. – Mtu yoyote mkazi wa Tanganyika akiwa Mzungu, Mhindi, Mwarabu au Mwafrika anaweza kugombea uchaguzi bila ya pingamizi yoyote, hali kadhalika atakuwa na haki ya kupiga kura. Kwa hiyo T.A.N.U. itakuwa na wajibu wa kuwaomba wanachama wake wakati wa uchaguzi ujao wawachague wageni wale waliokubaliwa na T.A.N.U. kugombea uchaguzi huo.*

Footnote 132, p.214, *Mwafrika*, Letter R.G. Siwale, 16th June 1958, p.2.

Waafrika wa Tanganyika si maadui wa mataifa ya Ulaya na hata Afrika nzima haina uadui huo na mataifa yote ya Ulaya. Waafrika wa Tanganyika wanapodai uhuru wa kujitawala wenyewe sio kwamba wanaudai uadui [illegible] na mgeni yeyote, la, ni desturi kama alivyoumba Mungu kila taifa na nchi yake lijitawale wenyewe, lakini sio kutawaliwa na wengine.

Mwenyezi Mungu kasema kuwa watu wote duniani wako sawa mbele yangu na hakuna aliyemshinda mwingine. Waafrika kutaka madaraka ya kujitawala ni namna ya kuonyesha ustaarabu wao, na kufuata maagizo ya Mungu.

Footnote 133, p.214, *Kiongozi*, Letter Alfons Mpiluka, 16th February 1959, p.3.

Wakuu wote wa Serikali wawe Waafrika Watanganyika wenzetu, yaani weusi kwa weusi. Kumbuka sasa Tanganyika ni mali ya Malkia (Uingereza), ba'i tukijitawala itakuwa mali ya Serikali ya Tanganyika. Basi Wazungu je? Watakubali kuwa chini yetu, yaani kuwa chini ya mtawala wa mahali pale akaapo kama raia wa Tanganyika?

Wengine wengi, itawapasa kuhama au tuseme kurudi kama walivyokuja kwa amani na kurudi pia kwa amani. Wengine watakaa na tutahitaji wengi kwa umaana wao.

Footnote 134, p.215, *Ngurumo*, Letter Charles Mugambi, 5th December 1960, p.2.

Waafrika wote walikuwa wakidhani kuwa tangu TANU ianzishwe ilikuwa ikitaka kuwapatia wananchi nchi yao waitawale, na kwamba Wazungu, Waarabu na Waasia watahesabiwa ni kama wageni tu.

Footnote 135, p.215, *Ngurumo*, Letter S.M. Kalason, 26th October 1961, p.2.

TANU ilianzishwa kwa kutaka UHURU wa Watanganyika (Waafrika). Misukosuko iliyotokea mpaka hatua hii ya leo sina haja ya kuyasema kwani kila mmoja wetu ayajua.

UTP ilibuniwa kwa madhumuni ya kutaka mseto katika nchi hii ya Tanganyika, na chama hiki kilikuwa kikiendeshwa na matajiri wenye mali (Wahindi na Wazungu) nia ya chama ilikuwa mataifa yote ya Tanganyika yawe sawa. Kwa bidii za Waafrika chama hicho kilizikwa huko kilikoanzishwa Tanga. TANU ikapaza sauti – Mseto ni haramu ya Tanganyika.

...

Wapenzi ndugu zanguni, wajuaji na wenye elimu mnaweza kuniambia ni nini tofauti ya TANU ya leo na UTP "ati" iliyozikwa? Federation itaruhusu mseto huo? Mzee Kenyatta ametuhutubia uongo aliposema watu weupe wawe chini ya utawala wa Waafrika? Je, mmeonaje huo uraia?

Footnote 138, p.216, *Ngurumo*, 28th October 1961, p.1.

Katika hotuba yake Bw. Tumbo alisema "Waafrika tulipigwa kofi shavu moja; tukanyamaza: sasa hatutaki kugeuza shavu la pili nalo lipigwe..."

...

"Mimi sitaweza hata kuuza Uafrika wangu hata siku moja. Niko tayari kuitwa Hitla, Verwoeld,na hata Kaburu. Lakini sikubali kuwa wafalme katika viraka.

"Nakubaliana kabisa na Bw. Nyerere aliposema kwamba sisi hapa tunakalia baruti, lakini ni nani anaweza kuizima baruti ile. Jibu, ni Serikali. Kwa kuwa Mwafrika hakubali kupigwa kofi shavu la pili, wajibu wa Serikali kuwaambia Wazungu, Wahindi waache ubaladhuli wao. Haya ndiyo maji ya kuzima baruti ile. Ama sivyo, italipuka.["]

Footnote 150, p.219, *Ngurumo*, Letter Ibrahim M. Mushaifi, 9th December 1961, p.2.

Bwana Mwinyi uelewe kuwa Mwafrika si kabila, kwani mtu yeyote kujiita Mwafrika kwa maana fulani. Mfano huko Tunis kuna Waafrika lakini rangi yao ni sawa na Wazungu, bali ni Waafrika. Misri nao ni mchanganyiko, nao pia ni Waafrika. Ikiwa huo Uafrika wa ngozi nyeusi na pua pana, basi huo si uafrika, bali ni ukabila fulani.

Uelewe kuwa Mshehimiwa Bwana Nyerere angedai Uhuru wa ukabila, nafikiri leo Tanganyika bado tusingeijua tarehe ya Uhuru itakapo tolewa. Lakini kwa vile njia iliyopitiwa ni njia iliyopitiwa na wote waliodai Uhuru wa nchi zao kama vile Ghana na nchi nyinginezo waliokwisha pata Uhuru wao.

Footnote 151, p.220, *Kiongozi*, 1st November 1961, p.6.

Taarifa hiyo katika Kifungu cha 15 vasema: "Kila mtu ana haki ya kuwa na nchi yake, wala hatanyimwa haki ya kubadili Nchi yake (awe raia wa Nchi nyingine)." Kifungu hiki kinaonyesha wazi kuwa mtu anaweza kuhamia nchi nyingine na kuwa raia wa nchi hiyo. Hii ina maana va kusema kwamba Mungu ameiumba dunia kwa ajili ya watu wote, ili wakae pamoja kidugu pasipo kubaguana huyu wa rangi nyeusi, huyu wa rangi kimanjano, huyu wa nywele za kipilipili. Wote tu watoto wa baba mmoja, Mungu.

Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa walipokutana Dar es Salaam tarehe 18 Oktoba kujadiliana juu Sheria mpya ya uraia iliyotungwa na Serikali, yaliotokea majibizano makali kuhusu hali ya baadaye ya wageni katika nchi hii. Baadhi ya Wajumbe waliipinga na wengine waliiunga mkono Serikali.

Sheria hiyo mpaya iliyotolewa na Serikali inasema kwamba Siku ya Uhuru tarehe 9 Desemba, watu wote wasiokuwa Waafrika katika Tanganyika ambao walizaliwa Tanganyika na asili yao ni nchi mojawapo ya Commonwealth na mmoja wa wazazi wao akiwa alizaliea Tanganyika, basi Siku ya Uhuru watu hawa wote watageuka kuwa raia wa Tanganyika.

Wajumbe fulani fulani walipinga kwa nguvu kabisa Sheria hii hata mmoja akasema "potelea mbali na Commonwealth." Alisema kuwa Sheria hii ikipitishwa Waafrika wataendelea kugandamizwa na Wazungu na Waasia kwa kuwa hawa wana maki tena werevu zaidi kuliko Waafrika.

Tunakubaliana na Mjumbe huyu kuwa Wazungu na Waasia wanampita Mwafrika kwa mali na elimu, lakini hii si hoja ya kumnyima uraia Mzungu au Mwasia anayependa kuwa Mtanganyika halisi, a kitupilia mbali uraia mwingine wowote. Hatuwezi kuvunja kanuni kubwa ya msingi (principle) sababu ya kuogopa kushindana na Watu weupe katika uchumi na elimu. Ile ngozi yao haiwafanyi kuwa na elimu zaidi.

Kununi ya msingi ni kwamba mtu hawezi kubaguliwa kwa ajili ya rangi yake. Kanuni hii inavunjwa na Serikali ya Makaburu huko Afrika ya Kusini, ambako rangi ndio kipimo cha uraia. Tanganyika ambayo imepinga ubaguzi wa rangi haiwezi kukubali uendeshwe kwa upande wa ndugu zetu weupe.

Moja ya madhumuni ya TANU ni kuondosha ubaguzi na kuupinga popote ulipo kwa kufuata Taarifa ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu.

Ni wazi kuwa Wajumbe waliopinga Sheria hiyo ya uraia walisahau madhumuni ya TANU. Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu aliwakemea kwa sauti ya ukali akisema: "Wajumbe wengine wanakuja humu Barazani wamelewa ukuu, wakitoa hotuba zisizo na maana na kutenda kama ma-Hitler. Hotuba zao zimejaa ubaguzi na uchukiyu kama hotuba za Verwoerd , Waziri Mkuu wa Afrika ya Kusini."

Tanganyika imetoa mfano mzuri kwa dunia yote kwa kukubali Sheria hiyo mpya ya uraia. Wajumbe walipopiga jura, wengi waliiunga mkono Serikali. Wakati Tanganyika itakapoingia katika Umoja wa Mataifa, itaweza kuipinga kwa haki Serikali ya Afrika ya Kusini isiyojali Haki za Binadamu. Itaweza kusema mbele ya mataifa yote ya ulimwengu: Njoni Tanganyika muone tunavyoheshimu uhuru na haki za binadamu. Kwetu ubaguzi wa rangi haujulikana. Waafrika Wazungu na Wasia tunashirikiana pamoja kidugu, tukiwa wote na uraia mmoja.

Footnote 152, p.220, *Ngurumo*, Letter A.L. Hassan Mkunge, 6th May 1961, p.2.

Chama cha upinzani kinachofuata ukabila dini au taifa hakifai kwani ni mzigo wa kinyume cha uswali wa uchi hii. Mpaka leo tunayo Serikali ya kujitawala kwa mambo ya ndani kwa ajili ya umoja wetu na hatukupoteza kichwa cha mtu kuutafuta uhuru huu.

Ningependa kumkumbusha Prime Minister kuwa Tanganyika ni ya Watanganyika hivyo kusiwepo na tofauti au hitilafu kufuata RANGI kwani juzi kwenye Serikali ya Mkoloni kulikuwa na kikundi ambacho kilifaidi sana maisha na kukifanya kikundi kingine si wanadamu. Leo sisi tuliokuwa tunafanywa si watu tumekubali kushirikiana na kundi hilo kutimiza maamri ya Rabuka.

Footnote 153, p.220, *Kiongozi*, *Uhuru Na Haki Tu?*, 15th February 1960, p.7.

Tanganyika kama vile nchi nyingine kuna makabila mengi ajabu na watu wa kila rangi – si weusi, si weupe. Watu hawa wanelekea kutengana, kubaguana na kuishi katika msuguano wa kila namna. Baada ya muda yatakuwa huru, lakini uhuru tu hautaleta amani kwa watu hao. Ni wajibu wetu mimi wa wewe kumkaribisha Mama Mpendo ili aje kuondoa tofauti zote hizo, atuonyeshe kama watu wengine ni watu kama sisi. Hapo ndipo Tanganyika itakuwa Taifa lenye kudumu na kufurahia amani.

Footnote 154, p.220, *Kiongozi*, Letter Balthazar Masalu, 1st October 1958, p.2.

Haki za binadamu zilindwe na Serikali inayojali sheria, na sheria ni jambo la lazima kuunda urafiki baina ya mataifa.

Footnote 155, p.220, *Ngurumo*, Letter J.S. Ngare, 15th June 1961, p.2.

Nichapie barua hii katika gazeti letu maarufu ili niambiwe mengi yanayonitatiza sana kwa vile tunavyolitamaka ama kuliandika Baraza la Tanganyika kuitwa Baraza la Taifa.

Ninavyofahamu mimi naona taifa ni kama vile Waafrika, hili ni taifa moja, halafu Wahindi taifa moja na Wazungu taifa moja na Waamerka taifa moja. Nikisema mataifa hapo maana yake mchanganyiko wa mataifa kama hayo yakichanganyika pamoja huenda kwa kuunda umoja wao kwa kushauriana mapendekezo ya aina yoyote na ndivyo lilivyo Baraza letu la Tanganyika. Ninashangaa sana kila mara kuona baraza letu linaandikwa Baraza la Taifa kana kwamba linatumika kwa taifa moja. Hivyo naomba nilekezwe vema kwa utulivu sio wale wahuni wanaojiandikia kutafuta mtukanano.

Haikosi kuna wasomaji wenzangu ambao nao pia hawaelewi vema na mgorogoro huu na hivyo mara tupatapo maelezo kamili ni ubora.

Footnote 156, p.220, *Ngurumo*, Letter "*Mjunguja*", 19th June 1961, p.2.

Kama alivyosema ya kuwa ni wengi wenye mshangao huo, lakini nadhani kama akifikiri sana, atatambua kuwa Taifa ni neno linalokusanya makabila mawili au matatu kuwa taifa moja katika nchi moja.

Kama vile Baraza la Taifa la Tanganyika kwa hiyo, nawaomba wasomaji wako wasichanganye Taifa na Kabila. Ama kwa kweli Baraza hilo lingitwa la Kabila. Hapo hata mini jamani ningekwisha

uliza, lakini neno Taifa ni kama kwamba au tuseme lina maana ya mkorogeko wa makabila kama vile tuitavyo chakula cha mseto likiwa jina moja lakini ndani ya mseto zimo choroko, kunde, na mchele.

Waheshimiwa walipokatiza neno Taifa sina shaka walieleza shabaha kama ya mseto, kwa hiyo Bw. Ngare neno Taifa lisikusumbue kwa kadri nilivyoeleza. Naelewa wazi kuwa jamaa wako mbioni kukujulisha zaidi.

Footnote 157, p.221, *Mwafrika*, Letter Joseph Leon Yawi, 16th April 1960, p.2.

Kuweko kwa vile viti maalum kunadhihirisha kuwa serikali ya Kilkoloni nia yake ni kujenga ubaguzi wa mataifa daima, maana inahimiza kuweko kwa wajumbe fulani ambao watasimana kitaifa. Serikali inapaswa sasa itangaze wazi kuwa hakuna taifa liitwalo Waasia au Wazungu au Waafrika katika Tanganyika bali kuna Watanganyika na ishikilie kuwa Tanganyika ni nchi ya kwanza katika ulimwengu kuanzisha taifa jipya katika karne hii ya 20 ambalo halitajali rangi wala dini au ubaguzi wa aina yo yote.

Footnote 163, p.222, *Ngurumo*, 24th October 1961, p.1.

Sheria ya uraia itaharakisha Africanisation alisema Bwana Nyerere wakati alipokuwa akihutubia mkutano wa Wazee Arnautoglu siku Jumaa Mosi.

"Kwa Sheria ya Uraia, alisema, nitaweza kujua ni nani ambaye kasimama mguu mmoja huku na mwingine huko."

Footnote 166, p.222, *Mwafrika*, 23rd January 1960, p.6.

Tabia ya kukaa chini na kuwa geugeu, alisema Bwana Nyerere ni tabia inayochukuzia sana wala haistahili mwanmume kufanya tabia ya namna hiyo ndio njia yake ya kupatia riziki. Bwana Nyerere alilaumu sana tabia ya Wahindi ya kukaa chini tu kuuza chumvi na dagaa au pilipili bizari na kusubiri tu watu waje kununua kitu hiki na kile, kwa hiyo, alisema, Tanganyika ya baadae itakuwa Tanganyika ya kazi isio na ubaguzi wowote, itabidi lazima kila raia wa Tanganyika bila ya kutofautisha rangi au taifa kufanya kazi kila inapobidi kazi za lazima za kuenesha maendeleo ya nchi mbele, kwa hiyo yeyote ambae anaetizima kukaa na kusubiri wakati wenzake wanafanya kazi huyo Tanganyika ya baadae haitamfaa anastahili kuondoka mapema.

Footnote 168, p.223, *Ngurumo*, 2nd December 1961, p.1.

Bwana Kahama akasema, "Nikiachilia mbali habari za sheria hii, nataka kuchukua nafasi hii kuondoa mashaka ye yote. Mashaka haya niyasemayo ni yale yaliyoelezwa na wajumbe waheshimiwa wengine wengine katika mkutano uliopita. Kuwa ikiwa wasio Waafrika wataruhusiwa kuwa raia, watatumia uraia wao kuwapokonya Waafrika ardhi yao.

"Naujua woga huu, japokuwa sisadiki ukweli ulioko nyuma yake kuwa Waafrika hawajiwezi na wajinga katika wakati wa kisasa kuwaruhusu watu wengine wawanyang'anye ardhi yao ambayo tongeapo kwa sheria wanaitumia.

Nimeamriwa na rafiki yangu kwamba Serikali haitazamii kubadilisha utaratibu wa sheria za ardhi; katika kutengeneza sheria ya uraia.

Kwa hiyo kubadilishwa ardhi, kutoka kwa Mwafrika na kupewa asiye Mwafrika kutaendelea kukatazwa.

Footnote 170, p.224, *Ngurumo*, 28th October 1961, p.1.

"*Ugomvi wetu sio kabagua watua wa mataifa ya kigeni. Tunachotaka ni ufalme katika nchi yetu. Huwezi kuwa Mfalme bila fedha. Anayetuita sisi tunashikilia ubaguzi, anakufuku Mungu."*

Alisema Bwana Kassanga Tumbo, Mwandishi Mkuu wa TRAU, jana jioni alipokuwa akiwahutubia wanachama wa vyama vya Waafrika katika idara ya Haikomisheni.

"Kwa sababu sasa uhuru unakaribia, alisema, tumeanza kuitwa wabaguzi. Waafrika tangu karne ya 18 walionyesha kuwa sio wabaguzi. Livingstone, mgunduzi Afrika, alikuja hana kitu. Maji pa kulala, chakula alikuwa akipewa hapa. Baadaye akafia hapa na Waafrika wakaubeba mwili wake mpaka makwao. Hii haikuwa dalili ya ibaguzi.

.... Kutulinganisha sisi kuwa kama Kaburu, ni kumkufuru Mungu.

...

"Mimi sitaweza hata kuuza Uafrika wangu hata siku moja. Niko tayari kuitwa Hitla, Verwoeld, na hata Kaburu. Lakini sikubali kuwa wafalme katika viraka.["]

Footnote 171, p.224, *Mwafrika*, Letter Mathiasi D. Masanja, 27th February 1960, p.2.

Mawazo yangu ni kuwa hawa jamaa wa Kiasia ndio sumu ya huu mgomo na migomo mingine. Hapa ningetaka kuuliza swali kwamba vitendo hivi kweli vinaweza kuunda lile taifa kuu la Watanganyika?

Mambo haya yanatuonyesha kuwa watu wengine wa namna hii wapo hapa kwa ajili ya faida zao wenyewe tu na wala si kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Hivyo naona kuwa Bwana Nyerere atakuwa na kazi kubwa ya kunyosha nyoyo za hawa jamaa.

Footnote 172, p.224, *Mwafrika*, Letter A.L. Kilenga, 25th April 1959, p.2.

Tafadhali naomba nafasi katika gazeti lako ili nizungumze na ndugu Waafrika juu fikara za Wazungu fulani, mara nyingi nimepata kusikia kwa hao Wazungu wakisema; "Wao walipendelewa na Mungu na hivyo ni Malaika wa duniani, hutoa sababu na kusema kuwa wamepewa akili nyingi na mwili wao ni mkubwa, na pia roho zai ni za imani zaidi, hivyo ni haki yao watawale na kutimikiwa na vijakazi (Waafrika) wetu tuliopewa na Mwenyezi Mungu." Ndugu zangu ebu fikirini juu ya msemo huu, ama kwa hakika wanajua sana kutusema. Je, huo mseto au mchananyiko wa Mataifa utafaa namna gani hapa Tanganyika ikiwa hali ilioko ni kama hiyo?.

Ajabu ingine ni kwamba, baada ya wao kufika huku Afrika na urafiki sana nasi, lakini baada ya siku si nyingi huwa wakiyufikiria kuwa labda sisi huwa si binadamu halisi, nao hutegemea siku zote Mwafrika apige magoti mbele yao na kuitikia ndiyo bwana. Mtoto wa Kizungu mwenye unri wa miaka saba hutegemea aitwe bwana na mzee wa Kiafrika mwenye unri wa miaka mia moja. Ajabu gani hiyo? Je wewe uitwaye kibarua utadanganyikaje ili utawaliwe na mseto.

Kwa maoni yangu mimi si halali kushirikiana na mtu asiyekuthamini, hivyo ni haki yetu kuwagomea ili tuwe na haki kama bindamu wengine.

Footnote 177, p.227, *Kiongozi*, 17th November 1959, p.4

Walakini tusijidanganye tukafikiri ni kazi nyepesi kujitawala. Ni kazi ngumu sana. Hao Mawaziri na wajumbe wetu kaitika Lejiko sherti wawe watu wenye busara, hodari kwa kazi, watu wenye uadilifu na maarifa mengi ili waweze kushika madaraka hayo makubwa.

Ni kweli kabisa kama zamani kabla ya Wazungu kuja huku Afrika tulikuwa tukijitawala. Lakini utawala wenyewe ulikuwa wa namna gani? Haukuwa na madaraka mengi kama ulivyo utawala wa kisasa. Hapakuwa na Education Department, wala Medical Department. Tawala zetu hazikuwa na uhusiano na tawala nyingine za nje ya Tanganyika, ambaopo sasa ni jambo muhimu kabisa kwa habari ya biashara, uchukuzi, simu, posta n.k.

Kumbe basi wakati tunapojitayarisha kupokea madaraka hayo sherti tutupilie mbali uvivu na uzembe. Tuwe watu wa kazi. Haitoshi kulia: uhuru, uhuru, sherti tufanye kazi zetu kwa bidii zaidi. Tuwanonyeshe wageni kwamba tunaweza kukabidhiwa madaraka hayo. Tukae tukijua kwamba mambo haya mawili: UHURU NA KAZI sherti yaende pamoja.

Wapo wanaofahamu maneno hayo Uhuru na Kazi kwa maana ya kusema sherti tufanye kazi ngumu kwa kupata uhuru wetu. Nasi twakubaliana nao, maana hao waliokuja kututawala hawataki kutupa uhuru wa kujitawala pasipo sisi wenyewe kuonyesha jitahada ya kuupata.

Walakini hata katika kutafuta uhuru sherti tuwe watu adilifu na wacha Mungu. Hatuwezi kutumia njia zisizo halali kwa kupata uhuru. Mkubwa mmoja wa TANU aliwahimiza wanawake wawasukume waume zao kutoka nje ya nyumba zao walimojificha kwa woga na kupigania uhuru. Mkpaka hapo si neno. Akaongeza lakini kusema kwamba waume hao wakizidi kujificha nyumbani ni bora kuivunja ndoa na kuwaacha. Hapo msemaji alikosea sana. Labda tuseme ulimi uliteleza tu; yeye hakuwa na nia ya kusema vile. Kama kweli alitaka kuwahimiza wanawake watende vile, wavunje ndoa zao kwa sababu ya uhuru, hapo alifanya kosa kubwa sana.

Hatuwezi kuvunja Amri ya Mungu kwa kutaka kupata uhuru, kama vile tusivyoweza kuiba pesa za watu ili tukamnunulie nguo mke au watoto. Yatupasa kuchuma fedha kwa njia halali. Na UHURU tuutafute kwa KAZI lakini kwa njia halali.

Footnote 179, p.228, *Kiongozi*, Letter Mwl. F.M. Marenge, 15th December 1959, p.3.

Ninawaomba watoto wote walioelimishiwa shuleni, washughulike na maendeleo ya nchi kuliko kuonyesha ujuzi kilabuni. Haina maana,. Ni upotezi wa maisha ya mbele. Tabia nzuri ndiyo ustaarabu.

Footnote 180, p.228, *Kiongozi*, Letter A.P. Hovyo, 1st March 1960, p.3.

Mimi nadhani kila liwalo la jadi lina sababu ya kutosha. Wakati lilipoanza kulikuwa na sababu ya kutosha ingawa labda baada ya miaka mingi kupita na mabadiliko kuwa mengi huenda sababu ya kuanzishwa jambo hilo zinaonekana za upuuzi. Naamini kabisa kuwa wahenga wetu walipoanza habari ya kutozana mahari walikuwa na sababu muhimu. Zamani mwanaume alipooa, alimpeleka

mkewe kwa wazazi wake. Hiyo ilimaanisha kuwa watu wa kuumeni walipata mtu mmoja zaidi wa kuwasaidia kazi zao. Vile vile wale wa kukeni walipungukiwa mtu mmoja na kwa hali hii kabala ya kufarakana na binti wao walitaka wapate angao pesa au mifugo kidogo, vitu ambavyo vitawasaidia kumalizia baadhi ya shida ambazo zimewafikia kwa kutokwa na binti wao. Zamani zile, na mpaka sasa, mwanamke akiolewa amekwisha hama kabisa kwa wazazi.

Ingawa sasa tulio wengi hatukai kwa wazee wetu tukisha oa, bali tunakaa na wake zetu mahali tufanyiapo kazi, hata hivyo wazazi wa watoto wa kike wanapungukiwa msada kwa kazi zao, waolewapo watoto wao. Siku hizi wasichana wanaelimishwa kama vile wavulana, kwa gharama ya wazazi wao. Wazee wa wavulana wanapata manufaa wanao waanzapo kazi ya mishahara. Wazazi wa wasichana na baada ya kutoa gharama za kusomesha mabinti zao hawaambulii chochote wasichana zao wakiolewa, hasa mara tu baada ya masomo yao. Sasa, Bwan Kapessa, huoni kuwa ni haki tu waombe mahari kama ushuru kwa gharama walizopata wawasomeshapo mabinti zao? Sina shaka unaelewa kwamba mke aliyeelimishwa anao ujuzi fulani fulani ambao akiutumia nyumbani mwake mumewe hustarehe kuliko mume wa yule mwananke asiye elimishwa. Sasa je, ukikombwa ushuru wa starehe hizo unaona kuwa unakosewa!

Footnote 181, p.228, *Kiongozi*, Letter Anne M. Ambrose, 15th February 1960, p.3.

Umekwisha sema kuwa bwana na bibi waendako kuoana watoe kiasi fulani cha fedha yaani kama ulivyokwisha sema Shs.350/- kwa kila mmoja, hata vile bibi ataambiwa mwba wee! Mpumbafu! Nenda kwenu sikutaki. Pia bwana atafurahi sana kwa mchango huo, yaani ataanza kufikiri mambo na mipango mingi itakayofanyika, mara utamsikia bwana akisema kuwa anataka kununua basikeli au redio. Bibi bila kusita atakubali, na baada ya muda bwana ataomba Shs.5/- kwenda kilabuni kununua pombe. Bibi akisema nataka nguo, bwana atasema angojee kidogo. Mvurugano ukizidi bwana atafoka: Nani mkubwa wewe au mimi? Hapo bibi ataanza kufanya matata na kusema mbona wote tulitoa kiasi cha fedha cha aina moja? Mbona mimi wanipunja vile? Kwa kushikwa na kuburi bibi atachukua kiasi fulani cha fedha kwa mafano yake. Kuona hivyo bwana ataanza kuchachamaa, na mara moja fujo tayari!

Footnote 182, p.228, *Kiongozi*, Letter D.C. Tibasima, 15th February 1960, p.3.

Nionavyo mimi, maharo yakomeshwe katika nchi hii ya Tanganyika. Mvulana na misichana wapendane mapendo ya haki tupu. Wakipata shida, wavumiliane, wakigombana wapatane, siyo huyu kusema naweza kwenda kwetu na ukarudishiwa mahari yako. Mapendano ni jambo ambalo linamaliza yote. Je, nyumba ngapi hasa kwa vijana utakuta matata ya kila aina? Je, yo yote hayo ni kwa nini? Ni kwa sababu ya uchoyo wa wazazi kutoza mahari.

Footnote 183, p.229, (a) *Kiongozi*, Letter P.D. Kapessa, 15th January 1960, p.3.

Mungu akwaweka Paradizini baada ya kuwabariki, na waliishi na ndoa yao takatifu ya kiasili. Je! ninyi wazazi wa wasichana nani kati yenu anayeweza kuniambia kwamba baba na mama wa Eve walipokea mahari kiasi fulani kutoka mkwe wao Adam? Na wazazi wa baba yetu wa kwanza Adam walilipa kiasi gani kumwoza mtoto wao Adamu? Napenda kuwafahamisha kuwa kuzaa ni amri ya Mungu, na wazazi wanapozaa siyo mali yao ila ni mali ya Mungu na zawadi yake, siyo kwamba mtu anapozaa huwa anaongeza uchumi nyumbani kwake. Wazazi wa watoto wa kike wasahau kabisa

kwamba kuwa wanazaa mali yao kwa vile huwa na matumaini sana wanapomwona binti wao karibu kutimiza miaka ya kuweza kuolewa, wakifurahi na kusema kuwa karibu watakuwa na biashara kubwa sana nyumbani pao, yaani watapokea mahari kutoka kwa mkwe fulani.

Haya ni mawazo yasiyo na maana hata kidogo, acheni kuuza mali na zawadi ya Mungu. Mkitaka kuwa matajiri fanyeni kazi kwa bidii zenu na Mungu atawasaidieni na atawapa mali lakini siyo kuuza mali yake....

Tunasema kuwa biashara ya utumwa ilikwisha. Hata kidogo; bado ipo tu.

(b) *Kiongozi*, Letter Lucas John, 15th February 1960, p.3.

Ni jambo lisiloleta ustaarabu kabisa, kumchukua mtoto wako wa kike na kumuuzuia mtu mwingine. Watu wengi hawaelewi kwamba kupokea mahari ni sawa na kumuuza mtoto wako, halafu baada ya siku mbili unakwenda kwa yule yule mkweo uliyemuuzia mtoto wako na kuomba pesa za kununua chumvi bila kuona haya. Hapo wazidi kuwanyanganya riziki zao.

Utumwa huu uliletwa na wazee wetu waliotangulia kwa kuwauza watoto wao wakifuata utumwa wa Waarabu.

(c) *Kiongozi*, Letter D.C. Tibasima, 15th February 1960, p.3.

Dokezo la Bwana Kapessa katika – KIONGOZI – ya tarehe 15 Januari ni dokezo la busara sana kwa mtu anayefikiri sana hali ya wanawake wa Kiafrika na hali ya ule utumwa wa ndugu zetu Waarabu ambao baada ya kuwauza babu zetu katika utumwa sasa tumekuwa ndugu kwa ndugu.

Footnote 184, p.229, *Kiongozi*, Letter D.C. Tibasima, 15th February 1960, p.3.

Mapendano ni jambo ambalo linamaliza yote. Je, nyumba ngapi hasa kwa vijana utakuta matata ya kila aina? Je, yo yote hayo ni kwa nini? Ni kwa sababu ya uchoyo wa wazazi kutoza mahari. Nasimama mstari mmoja na Bwana Kapessa mahari yakomeshwe, na badala yake pande zote mbili zitoe vifurahisho vya maarusi kama zawadi kwa watoto wao. Naam, zawadi hizi kama ni fedha au vitu vingine, uwe ni msingi wa kudumisha mapendano yao, na hapo tu ndipo vijana wetu wa Tanagnyika watathamini ndoa zao na kuishi kwa raha mume na mke.

Footnote 185, p.229, *Kiongozi*, Letter '*Msichana Mwenye Uchungu*', 1st April 1960, p.3.

Mimi mwenyewe nilimpenda kijana mmoja. Alipofika kwa wazee wangu aliambiwa atoe Shs. 400/-. Maskini huyo kijana alikuwa hana baba wala mama; wote walikwisha kufa. Kwa hali yake hiyo alishindwa. Nilipoambiwa kuatafuta mchumba mwingine nilikataa kwa sababu baba alitaka mahari kuliko kunithamini mimi. Yule kijana tukaachana hivi hivi tu kwa sababu ya hayo mahari.

Jambo hili la mahari hasa linadumisha umalaya kwa wasichana hata kwa wavulana pia. Kwa mfano watu wa ndoa wakiisha achana, bwana atakwenda kwa wakwe zake kudai mahari. Kama hawana mahari ya kurudisha itawala zimu wamshurutishe binti wao kurudi kwa mume wake. Binti pengine atatoroka na kwenda mijini kuanza umalaya. Je, ni kosa la nani? Wazazi wetu nawaomba mtusaidie na kufikiria sana jambo hili. Mtoto wa kike na wa kiume mnawazaa wenyewe. Ya nini kuuza mmoja wao?

Footnote 186, p.229, *Kiongozi*, Letter Alexander Kasikila, 1st April 1960, p.3.

Kwa mwisho kabisa, mimi nasema: "Mahari ni chanzo cha wahuni, haramu, makauboi, wezi, malaya na kadhalika. Shime shime wazee watu litupieni macho makali jambo hili. Sisi twangojea kwa hamu tarehe ya kutangazwa mwisho wa mahari.

Footnote 187, p.229, *Kiongozi*, Letter K.N.K. Mndeme, 15th March 1960, p.3.

Mahari ni chanzo cha uhuni, wizi na usherati. Asante kwa maoni Bwana M.D. Masanja. Vijana wengi hupata kuwa hivyo kwani hawana wake. Kwa nini hawana wake? Kwa sababu hawana mali ya kulipa mahari. Kijana aishapo kuoa ni wazi atatafuta kazi ya kutunzia jamaa yake, mke, n.k. Lakini ebu waone akina yahe bila wake. Hushinda wakiranda ovyo wakijifikiria upekee ambavyo no rahisi kuliko akiwa na jamaa yake. Hapo shetani humpa kazi. Hili ni kosa kuu la nani? La mzee Maganga auzaye mtoto wake. Samahani wazee, lakini hili ni jambo la kusikitisha. Je, ungetoa mwanzo bure na kumzawadisha, hungeheshimiwa zaidi kuliko kumsababisha kijana mmoja kuwa mwizi?

Kwa jumla naona mahari yale kabisa, yaitwe marehemu U.T.P.; yabaki mapatano kati ya wazazi baada ya watoto kupendana. Hapo basi na uhuni utapungua na nchi yetu itaendelea na tabia nzuri. Kwetu vijana wote tukatae kuoa au kuolewa kwa mahari, na mzee atakayeng'ang'ania mahari asuswe, yaani vijana wasioe au kuolewa kwake. Hii na dawa nzuri ya kukomesha baa hili.

Footnote 188, p.229, *Kiongozi*, Letter Bi. M.A. Kiondo, 15th October 1960, p.3.

Tujitahidi sisi wenyewe kupunguza mizigo mizito miwili – ULEVI na UMALAYA. Hawa ni ndugu pacha.

Footnote 189, p.229, *Mwafrika*, Letter Sefu S. Mohamed, 17th September 1960, p.2.

Kila mara siku hizi husikia kuwa wanawake wanafanya umalaya hadharani wamekamatwa na kufikishwa mbele ya baraza za hukumu. Wengi wao huwa wamekamatwa na kufikishwa mbele za baraza za hukumu. Wengi wao huwa wamekamatwa na wale watu wanaoona fedheha wanawake wa taifa hili la Kiafrika kufanya mambo machifu hadharani.

Kwa hakika ningependa kutoa shukrani kwa makorti wa wakuu wa mabaraza ya hukumu kwa kutoa adhabu kwa wanawake hawa. Lakini ningeomba kuwa hukumu iongezwe kuwa kali zaidi. Kama adhabu ya kifungo ikiwekwa naamini umalaya utapungua sana. Lakini ikiwa ni faini tu, umalaya utazidi maana malaya wanafahamu njia nyingi za kupatia fedha.

Footnote 190, p.230, *Kiongozi*, Letter B.K. Kiberenge, 15th October 1960, p.3.

Nadhani TANU itakubaliana nami kuwa ni fedheha tupu kuona raia wa nchi yetu wanauza miili yao.

Footnote 191, p.230, *Kiongozi*, Letter Nicolas B. Masali, 15th October 1960, p.3.

Kweli maneno haya au njia hii huenda ikawa ni njia mojawapo ya kukomesha hao malaya wasiendelee kuharibu sifa ya Taifa letu la Tanganyika.

Footnote 192, p.230, *Mwafrika*, 8th April 1961.

Chifu Francis Masanja MLC wa Kwimba amewakemea sana wananwake malaya wanaotembea ovyo hadharani, mahali pa watu wote wa na mahaa kwamba wanavunja heshima ya Kiafrika na kuifedhehesha nchi.

...

Andai kwambwa wanawake wa Kiafrika wanakwenda bar ambaopo wanakubali kufunuliwa nguo au kufanyiwa malendo machafu na yasiyopendeza watu: "Jambo kama hili lazima lifikiriwa sana na Serikali maana linavunja heshima ya nchi hii" alisema.

Footnote 194, p.230, *Kiongozi*, Letter "*Ni aibu sana bwana*", May 1957, p.4.

Bibi Helena, nadhani ulipotaka kumjibu Bwana Msezawe hukusoma kwa makini lalamiko lake juu ya mavazi ya wasichana. Bibi Helena nataka ujue kuwa ustaarabu hauji kamwe kwa kujipamba kwa sketi au mivauli; wala hata tai kwa full suit. Tukiangalia sana tunaona kuwa mivao hii yote imekuja katika karne za siku hizihizi – kumbe sisi sote tunaiga tu. Tutembee kwanza kidogo duniani, na ni mtembeze bibi Helena aone kuna nini. Bibi Helena unajua kuwa Gold Coast haijaacha kamwe ule mvao wa kiasili – shuka au lubega? Niambie, ustaarabu wao na huu wa Tanganyika ukoje? Hujo Uhindi mila zao wamezishikilia kikweli kweli. Uingereza nako kuna mvao ka kipekee lakini haijatokea hata mara moja kumwona Memsabu wa Kizungu amevaa Buibui na kuipania magotini, na tena isitoshe Bibi Helena, hakujatokea hata mara moja kumwona mama wa Kizungu akienda kanisani (nyumba ya Mungu usiifananishe na sherehe ya arusi kama ulivyosema) amevaa simizi huku macho yake yakiwayawaya huko na huko kanisani.

...Ni ajabu kidogo, na ajabu hii hutendeka kila mahali mijini: Dansi kina dada hujikwatua kwa mivao mbalimbali ya migandio, miavuli, na kadhalika, mavazi hubururwa chini, lakini katika nyumba ya Mungu hujipamba kwa nguo fupi fupi, niseme wazi – kama chupi . Lipi bora: Nyumba ya Bwana au Welfare Centre? Kama dansini kina dada mwavaa nguo ndefu, kanisani vaeni nguo ndefu mara mia kuliko kuvaa hizo nguo za magotini. Atasemaje mgeni mtoka India au Amerika au Ulaya akiona hayo Kanisani? Haya tupu...

... Ndiyo – ingawa si Pasaka hii, lakini Noeli ijayo, Msezawe K. Msezawe na mimi (na wale wapendao Tanganyika kujistahi) tutafurahi na kuwapa heshima kina dada Wakristu tukiona mmerefusha mavazi yenu wakati mtakapokuja kumwabudu KITOTO YESU.

Footnote 195, p.231, *Kiongozi*, Letter J.B.A. Rugeihyamu, 15th October 1960, p.3.

Malaya ana uharibifu wa aina nne. Huuza miili yao, huleta magonjwa ya kila aina, huwa wavivu kwa kukaa tu bila kazi, na mwisho ndoa za watu huvunjwa na malaya.

Footnote 196, p.231, *Kiongozi*, Letter B.K. Kiberenge, 15th October 1960, p.3.

Malaya ndiyo asili ya maovu mengi. Malaya ni wevi, wanyang'anyi, wachawi, wenye magonjwa mabaya ya kusikitisha, ni wanyang'anyi wakuu na wadanganyifu.

Footenote 197, p.231, *Kiongozi*, Letter Mwl. Y.Z. William, 15th October 1960, p.3.

Neno hili la kukomesha umalaya hata mimi naona ni jambo la maana sana. Akina mama hawa wanaotumia jambo hili ni wazi kabisa wanaitukanisha Tanganyika yetu penzi. Kina mama kumbukeni sana Tanganyika yetu kwanza ilikuwa inaugua. Hatukudhani kama itatibiwa na kupata uzima. Sasa enyi akina mama, kwa kupona Tanganyika tumshukuru nani – Shetani au Mungu? ... Watoto wangapi mama umepoteza ambao wangeongeza hesabu ya watu wa Tanganyika yetu?

Footnote 198, p.231, *Kiongozi*, Letter Ramadhani R. Itabangura, 15th October 1960, p.3.

Mimi ni mmojawapo ninayechukia umalaya. Malaya hawa ambao huzurura mijini na kunyang'anya fedha za watu, naona inafaa waondolewe kabisa katika nchi hii ya Tanganyika. Ni watu wanaoharibu nchi, na magonjwa wa kila aina ya usherati hutokana nao.

Footnote 199, p.231, *Kiongozi*, 15th November 1960, p.4.

Mmoja wa wasomaji wetu ambaye ni Sheikh wa Kiislamu alitoa mawaidha yake akisema: "Jambo hili lifanyiwe mkazo mkali kwa kuondolewa mapema kabla ya mgeni wetu UHURU. Kwa hiyo wake kwa waume wasitawishao jambo la umalaya wafanyiwe msukosuko. Hasa wanaume wakionekana katika majumba ya wamalaya washtakiwe na kupewa adhabu kalikali. Baada ya wanaume wakina dada waletewe karandinga, watiwe nguvuni na kurudihswa makwao."

Footnote 200, p.231, *Kiongozi*, Letter A. NJ. Mabula, 17th October 1959, p.3.

Basi hima wazazi wenzangu, tushikane bega kwa bega kuijenga Afrika ya kesho, maana inatutegemea.

Footnote 201, p.231, *Mwafrika*, Letter Idi A. Salimu, 15th October 1960, p.2.

Ni jambo la kufurahisha sana kusikia kuwa Tanu Youth League inataka kuondoa malaya na wahuni wote katika miji yote ya Tanganyika na kuwapeleka makwao au kuwapa kazi za kulima. Hii inaonyesha hatua mojawapo ya kusafisha nchi na kuondoa fedheha kubwa ambayo Mwingereza ameshindwa kuiondoa muda wote alipokaa hapa.

Footnote 202, p.231, *Kiongozi*, Letter J.B.A. Rugeihyamu, 15th October 1960, p.3

Madaraka tuliyopata yawe kama kifagio cha kufagilia taka taka na mambo machafu kusudi mgeni wetu Uhuru asikute nchini humu mambo ya aibu kama hayo ambayo ni kinyume cha Tanganyika ya kesho.

Footnote 203, p.232, *Kiongozi*, 15th October 1960, p.3.

Na Tanu ikifaulu kuondoa umalaya tutaikiri sote kuwa kweli ina nguvu nchini.

Footnote 204, p.232, *Kiongozi*, Letter B.K. Kiberenge, 15th October 1960, p.3.

Nionavyo mimi jambo hili la Umalaya likichukuliwa na TANU litafanikiwa bila shaka. Umalaya hauwezi kushinda TANU katika Tanganyika.

Footnote 205, p.232, *Kiongozi*, Letter Stanislaus K. Mutahyabarwa, March 1958, p.2.

Afrika kama Ulaya, dini inahitajiwa ili iwe msingi wa maendeleo bora.

Footnote 206, p.232, *Kiongozi*, Letter '*Mtanganyika*', March 1957, p.4.

Ewe Mtanganyika, zingatia dini yako. Dini ndicho kiini cha mema yote, dini kwanza, na mambo ya kujitawala baadaye.

...

Pia watetezi wa Tanganyika wawe macho sana, kwani ni kazi bure kuunda chama cha utetezi bila kuwa na msingi wa dini.

Footnote 215, p.234, *Ngurumo*, 19th January 1961, p.4.

Katika hotuba yake ndefu Mheshimiwa Bw. Nyerere aligusia habari za kukopa fedha kutoka nchi za nje. Akasema kwamba kukopa ni kubaya, kunaitia nchi dhamana. Kila tunapokopa tunapunguza sehemu ndogo ya uhuru wetu. Njia moja tu ya kuendeleza nchi ni kufanya kazi, kufanya kazi, kunfanya kazi.

Footnote 218, p.235, *Ngurumo*, 3rd April 1961, p.1.

Kama Bwana Barango alivyowaambia watu jana kuwa Ngurumo bila shaka ataeleza yote ya jana, basi Bwana Nyerere alisema hivi:

"Wale ndugu zangu wanozurura nawaomba waache, waache kwa sababu ni vibaya, tena ni kufuru; twende tufanye kazi.["]

Footnote 222, p.235, *Mwafrika*, 24th September 1960, p.3.

Kikundi cha Tanu Youth League, wilaya ya Itigi, kilipokutana hivi karibuni kilitilia mkazo maazimio ya mkutano wa Tanu Youth League wa Dodoma kuhusu wanawake malaya na wahuni. Katika kuunga mkono azimio hilo, Youth League imesema kuwa wanawake watakaokataa kufanya kazi ya kilimo na wahuni wasio na kazi watarudishwa kwao ambako watakwenda kutemeba.

Footnote 224, p.236, *Kiongozi*, Letter A.T. Mgomberra, 15th February 1960, p.3.

Uhuru u karibu kwisha ndiyo kusema utapatikana hivi karibuni, lakini kazi je? Ni ya milele.

Footnote 225, p.236, *Mwafrika*, Letter Antony Mtunguja, 16th April 1960, p.2.

Uhuru hautaleta chochote zaidi kama hatutajitahidi kufanya kazi kwa mikono yetu. Uhuru ni shoka, kama alivyokwisha sema Mheshimiwa Bwana Nyerere. Na shoka mtu akipewa asitumaini kuwa litajichukua lenyewe liende porini kukata miti, au mtu akipewe jembe litajiinua liende shamba kulima. Bidii ya kuutumia uhuru ndiyo italeta mafaniko tu.

Footnote 229, p.237, *Ngurumo*, 19th January 1961, p.4.

Nia ya Serikali ni kuwasomesha watoto wote kwa muda usiopungua miaka minane yaani mtoto akiingia darasa la kwanza asitoke mpaka afike darasa la nane.

Hivi sasa watoto wanaosoma shuleni ni 44 katika kila watoto mia moja nchini, wale 56 kuwaendi shule na wanakwenda kaburini blia kujua hata a-be-che. Katika hao 44 wakifika darasa la nne wanachujwa na wachache tu wanaingizwa darasa la tano. Na hao wakifika darasa la nane wanachujwa kuingia la tisa, na hao nao wakifika la kumi wanachujwa tena kunapatikana wachache tu wanaofika darasa la kumi na mbili.

Tumeahidi kwamba tuwasomeshe watoto wote lakini kumbe tukitazama fedha za Serkali ni pauni milioni 25 amabzo zinahitaji kugawanywa kwenye idara mbali mbali. Idara ya elimu kama ikitaka fedha nyingi sana na pauni milioni tatu na nusu, ikiwa tunataka kutumia zaidi ya pauni hizo milioni tatu unusu, tuwe tayari kwamba watu watakosa kwinini, watakosa maji ya kunywa. Lakini pia hizo milioni tatu zikipatikana zina njia nyingi.

Footnote 230, p.237, *Ngurumo*, 19th January 1961, p.4.

Tutafanyaje kupata fedha nyingi zaidi za kuendesha shuguli zote hizo. Ni kuongeza mfuko wa kila mtu ili kuipatia Serikali fedha ya kuendeshea mambo ya nchi.

Alipoeleza jinsi ya kuongeza mfuko wa kila mtu Bw. Nyerere alisema hakuna njia nyingine yoyote ila kuongeza mpunga nchini, kuongeza kahawa nchini, kuongeza pamba nchini ili kunenepesha mifuko ya watu. Hii ndiyo njia peke yake.

Footnote 232, p.238, *Mwafrika*, Letter Sefu S. Mohamed, 17th September 1960, p.2.

Njia nyingine ambayo naiona ingefaa kupunguza malaya waliojaa mijini ni kuwahamisha wanawake na wahuni wote wasio na kazi katika miji na kuwapeleka mashamba ambapo watakwenda kufanya kazi za kilimo. Kama njia hii ikitumiwa itasaidia sana. Maazimio ambayo yametolewa na Tanu Youth wa Jimbo la Kati naamini yakisaidiwa, umalaya na uhuni utapungua katika jimbo hilo na itakuwa mfano wa kufaa kwa sehemu nyingine Tanganyika. Mimi ningeomba Tanu Youth League nchini pote wapitishe azimio la aina hii, nalo litiliwe shime na polisi, ili nchi yetu ambayo inapata uhuru isifedheheshwe na kitu hiki "Umalaya".

Footnote 233, p.238, *Mwafrika*, Letter Idi A. Salimu, 15th October 1960, p.2.

Ingawa kweli ni jambo la kufurahikia kuona malaya wanakatzwa kuishi katika miji katika Jimbo hili la Kati, lakini lazima pia tufikirie njia ya kufanya nao ili wapate kuishi. Nikisema hivyo nina maana ya kusema kuwa hao wahuni wapewe kazi ili iwape kula na kuishi kama watu wengine. Pia hao wanawake malaya wapatiwe kazi ambayo itakuwa badala ya umalaya. Ama sivyo sioni kuwa jambo ambalo linashikiliwa na Tanu Youth League la kuwaondoa wahuni na malaya katika miji na kuwapeleka kwao litasaidia kitu sana katika Tanganyika.

Footnote 234, p.238, *Kiongozi*, Letter B.K. Kiberenge, 15th October 1960, p.3

Kila mtu ni lazima apate ridhiki yake, kwa jasho siyo kujiuzauza hivi. Siyo kwa kupiga uvivu na kuiba fedha za wengine bila haki.

Footnote 235 p.238, *Mwafrika* Letter J.R. Kallinga, 4th June 1960, p.2.

Inaumiza sana kuona kuwa wanaume tu ndio wanalipa kodi ingawa wanawake ni wengi kuliko wanaume.

Utakubaliana nami kuwa wapo wanawake wengi sana ambao wanafanya kazi na wanpata mishahara sawa na wanaume. Lakini hata hivyo hawalipa kodi yo yote Kuna wanawake wasio na kazi na pia wanaume wasio na kazi, lakini mwanamume asiye na kazi kuwa anadaiwa kodi, kwa nini mwanamke mwenye kazi asilipe kodi?

Katika nchi zilizoendelea au zinazotaka kupata fedha za kutosha kuendeleza uchumi na mambo ya serikali wanawake wenye kipato hutoswa kodi ya mapato, kwa hiyo Tanganyika sioni sababu wasitozwe kodi wanawake.

Footnote 236, p.239, *Kiongozi*, Letter Mwalimu Pius W. Luoga, 1st October 1960, p.3.

Nimekuwa na dukuduku sana juu ya utozaji wa kodi kwa upande mmoja tu yaani wanaume. Mara nyingi nilijiuliza, "Kwa nini wanawake hawalipi kodi?" Sikuweza kupata sababu zozote zilizonitosheleza za kuwasamehe wanawake wasilipe kodi ingawa wanayo kazi nzuri.

Nimeona hakika yawapasa walipe kodi kwa sababu kadhaa. Nitaona mfano moja. Bwana Juma ni mwalimu wa M. School fulani, anaishi pamoja na Bi. Mwal. Tausi afundishaye Girls' M. School ya jirani. Hawa wote ni walimu wa daraja ya kwanza na mishahara yao ni namna moja; nao wote hupata mishahara itokanayo na mapato ya kodi. Kwa nini basi Bwana Juma alipe kodi na Bi. Mwalimu Tausi asilipe?

Hawa waweza kulipa kodi za nyumba zao walizojikodisha, kodi za redio, za magari yao, za vyama na k.w.k. Je! Watashindwa kulipa kodi ya kichwa tu?

Ama kuna sheria ulimwenguni pote inayowahurumia wanawake wasilipe kodi ya kichwa?

Je! Fedha ngapi za namna hiyo zinaachiliwa kwa hawa wenzetu kama walimu, mabibi makarani, mapolisi, waganga na wauguzaji n.k. Bila shaka serikali yetu ingekuwa na lundo kubwa la fedha kuliko lilivyo sasa, kama ingekusanya kodi hawa wenzetu.

Vyeti vyao kodi vingeandikwa KODI ya MUDA kwa sababu ingewapasa walipe kodi hadi wakati wanapojiuzulu kazi yao.

Footnote 237, p.239, *Mwafrika*, Letter Gerson M. Manyau, 25th June 1960, p.2.

Ikiwa sheria hii itahimizwa italeta manufaa kwa njia mbili. Kwanza itwafanya wanawake wengi wasiopenda kuolewa waolewe ili wakwepe kulipa kodi, pili itafanya kupunguza wanawake wasio na kazi na walio na fikara kwamba mahali pazuri pa kujificha ni mjini ili wangojee wenzao kutoka mashamba walete mavuno ya jasho lao nao wale wamekaa.

Juu ya hapo hii ni njia mojawapo ya kuongeza utajiri wa serikali na chanzo cha kupata hospitali, shule, na elimu njema Tanganyika.

Footnote, 239, p.239, *Ngurumo*, Letter Theobald N. Msenga, 8th December 1961, p.2.

Waziri wa Fedha anastahili pongezi kubwa kwa barua yake hadi kufikia hatua kuwa, wanawake wasio na waume, na walioachika na waume zao, walipe kodi sawa na wanaume tangu tarehe 1.1.62.

Tunaomba sheria hii ingepitishwa na Wajumbe wa Taifa bila kungwa. Kati ya dada zetu wengine itawashinda kodi hiyo na itawalazimu kuolewa ili hiyo kodi isimpate na kwa hali hiyo, Malaya wengi ambao hututia aibu na fedheha na ambao jamaa wengi wamewapigia kelele magazetini watapungua. Na wale watakaoolewa hawawezi kuachika ovyo ovyo kwa kuogopa hiyo kodi.

Footnote 240, p.240, *Mwafrika*, Letter Rashidi Hamdani, p.2

Bwana Manyau ameleza kwamba wanawake wakilipa kodi basi wengi wataogopa kuishi mijini na watakwenda shamba wakalime; hiyo itakuwa njia mojawapo ya kupunguza umalaya katika miji. Hii ninapinga na kusema kwa uhakika kama wanawake wakifanywa kulipa kodi ni njia mojawapo ya kuwapa vyeti vya kuendeshea umalaya.

Ninasema itakuwa tumewakatia leseni za umalaya maana mwanamke abaye anafahamu kuwa anatakiwa alipe kodi atapita juu chini ili apate fedha za kulipa kodi. Je fedha hiyo ataipata wapi ikiwa kazi hana? Jibu liko karibu ni kuwa atafanya umalaya.

Footnote 241, p.240, *Kiongozi*, Letter Damian Chokunegela, 15th November 1960, p.3.

Je, unayajua maisha ya familia za Kiafrika Mwalimu? Nakuachia hapo ufikiri.

Chapter Four

Footnote 25, p.249, *Jicho*, 20th March 1957, p.1.

Katika hotuba yake [illegible] ya mashangilio makubwa, Bw. Argwings-Kodhek aliwasisitiza wasikizaji wale Waafrika kujitayarisha kuwa kujitawala Kenya.

Footnote 27, p.250, *Baraza*, Letter Lesingo Ole Keiuna, 15th April 1960, p.4.

Hata uhuru ukija sidhtrani kuna nafasu kwa makabila mengine kuishi katika nchi wa wamasai ata kuwa ni kubwa na kuna nafasi ya kuishu humo. Hata kuna watu wengine, wasioelewa mambo na hivi nao husema kuwa Wamasai hawaelewi kitu hata kidogo juu ya uhuru wa Kenya, sisi tunafahamu kabisa juu ya uhuru na tunautaka sana, ila si kwa njia ile wale watu wengine wanaotafuta.

Footnote 39, p.254, *Jicho*, Letter P.T. Kamau Karanja, 25th September 1957, p.6.

Sisi mabwana wengine ambao hufanya kazi mbali na nyumbani kwetu risavu, twahofia sana hali ya wale mabibi wafanyi kazi Nairobi. Wengine mabwana wanawangojea risavu, lakini barua hawajibu kamwe.

Footnote 41, p.254, *Jicho*, Letter Victor L. Omolo, November 1957, p.3.

Naam, fika hapa Mombasa, utakapoona wasichana wengi ambao baada ya kuingilia maisha ya mjini, hata hujiita wa-makabila mengine. Hivi watu huuliza: Je, kabila gani hili linaloruhusu wanawake kuharibika namna hii? (Sitataja makabila yao!).

Footnote 42, p.254, *Jicho*, Letter Kassan A. Amiri, 25th September 1957, p.6.

Wanaotoroka mabwana risavu na kuja hapa mijini kwenye ulevi, ni wale wavivu tu. Tulipojichagulia njia ya maendeleo na ustaarabu, ni kama tulitia kiberiti kwenye nywele zetu. Poleni basi!

...

Tabia hasa twahitaji kwa wale wasichana wote wa Kiafrika. Ni aibu kuwaona wengine wakijisemesha Kizungu kwenye 'bar', hali hawajaona wasichana wa Kihindi ama wa Kizungu wenye umri wa miaka kama 15 wakiingilia ulevi kwenye 'bar' na kuaibisha watu wa mataifa yao.

Footnote 123, p.276, *Jicho*, Letter *Pole Ashara*, 25th May 1960, p.3.

Vyama vya siasa kutegemea ukabila heri vipigiwe marufuku. Nasema hivyo baada ya kuchungua hali ya siasa ya nchi nyingi. Nchi ndogo kama Kenya haistahili kuwa na vyama vya ukabila siasani kwani hiyo itakuwa chanzo cha kuangamiza umoja nakualika wakoloni kutawala daima.

Hatutaki vita vya ukabila kuanza mara tu Wazungu wakitupa uhuru. Hakuna kitu kingine ambacho siasa italeta isipokuwa damu.

Foonote 162, p.283, *Jicho*, Letter Kai Ole Kiloit, 25th May 1960, p.3.

Pia hapendelei uongozi wa Mzee Jomo Kenyatta. Sioni kwa nini Mwafrika anayejidai kiongozi angesahau Baba wa Taifa la Kenya, Mzee Kenyatta ambaye alikuwa anatetea kila kabila, na kabila la Towett pia, hapa nchini Kenya, hata mbele ya kuzaliwa kwake.

Footnote 167, p.286, *Taifa Leo*, 9th January 1961, p.1.

"Kwa jumia," Bw. Muliro aliendelea, "KADU chatazamia kuwapatia wananchi uhuru wa aina mbili yaani uhuru wa kujitawala wenyewe na uhuru wa uchumi – ili Kenya idumishwe na kama sivyo itachafuka."

Footnote 186, p.290, *Taifa Leo*, Charles K. Mulela and two others, 27th February 1961, p.3.

Sisi sasa tunachoka kabisa na watu wa makabila mengine ambao wanasema ati walileta uhuru katika nchi hii. Watu hawa wanashikilia kwamba wamepigania uhuru na kwamba uhuru ukija watatawala nchi hii, wakiwa ndio viongozi.